# Pambazuko

Toleo Namba 152 | Jumatatu, Januari 26- Februari 1, 2026


# ‘Tukosoane, tusitekane, tusiuane’

Uk. 6&7

- Ni kauli ya Zitto akimlilia Mzee Mtei
- Mbowe: Serikali irekebishe makosa
- Mwigulu: Tutaendelea kumuenzi Mtei


Dkt. Nchemba


Mbowe


Zitto


Mtei

## Pazia Bima ya Afya kwa Wote kufunguliwa leo

Uk. 17

## Aliyevamia eneo la wazi, bado ‘akomalia’ ujenzi

Uk. 25



### Jicho la Tai

## Huyu mbunge aache kuwa mtoto

MIMI mzee wenu nilianza mwaka huu kwa furaha, licha ya kuchukizwa na mazonge ya mwaka jana – yale ya wakati wa uchaguzi mkuu na siku chache baadaye.

Safu Uk. 5

## Tanzania kuumia Marekani ikijiondoa WHO

Uk. 22



## Tahariri

# Ni wakati sasa kuponya taifa letu

TANZANIA ipo katika wakati muhimu wa kisiasa na kijamii unaohitaji busara, uvumilivu na utashi wa uongozi unaosimamiwa na ukomavu wa historia yetu.

Katika muktadha huu, ni jambo la muhimu kuhimiza haraka mchakato wa maridhiano kati ya vyama vyetu, taasisi na umma ili kuondoa kabisa dalili za uhasama zinazoonekana kukua siku hadi siku.

Uhasama huo hauumizi tu mazingira ya kisiasa, bali pia unaathiri maendeleo ya kiuchumi, amani ya jamii na kuaminiana kwa baadhi ya taasisi za serikali kwa umma.

Ieleweke kuwa vyama vinapaswa kuweka kipaumbele mazungumzo ya wazi na ya kujenga, siyo yale ya kushinikiza hasira wala kuendeleza aibu.

Maridhiano yenye maana yanahitaji kujenga msingi wa kuzungumza bila masharti magumu, kutambua makosa yaliyopita, na kujenga mikakati ya pamoja ya kuzuia migogoro inayoweza kutokea siku zijazo.

Hii inamaanisha pia kutangaza ahadi za uwazi katika mchakato wa mazungumzo, ili wananchi waone ni kwa jinsi gani mabadiliko hayo yanavyotekelezwa na kuwa na fursa ya kuyafuatilia kwa uwazi.

Taasisi za umma ikiwamo vyombo vya kutenda na kutekeleza haki, sheria na mashirika ya kiraia zinapaswa kusaidia kutuliza hali kwa kuhimiza ushirikiano badala ya kugawanya na kuhimiza kufanya kazi kwa haki na kutenda inavyotakiwa.

Na sisi vyombo vya habari tuna jukumu kubwa la kuleta taarifa sahihi, kuepuka uandishi wa chuki na kuchochea uhalali wa kila habari inayofika kwa umma kuwa yenye manufaa, hata kama ikiwa ni kuikosoa serikali na viongozi wake.

Vyombo vya sheria vinapaswa kutumika kama dhamana ya uamuzi wa haki pale migogoro inapotokea, bila kujali msimamo wa kisiasa wa pande husika.

Viongozi wa vyama wanahitaji kuonyesha uongozi wa uthubutu, kwa maneno na vitendo. Lugha ya kuchochea na vitendo vya kuzuia mazungumzo vinapaswa kuepukika kwa sasa.

Hawa viongozi wetu wanastahili kuonyesha mfano wa kuomba msamaha pale makosa yemetendeka, na kuonesha utayari kwa mashauriano ya kusamehe pale walipoumizwa na kueleza wazi nao waliumiza wapi na kwa kina nani.

Wananchi nao wanapaswa kushirikishwa katika mchakato wa maridhiano, kwani yanapowashirikisha, hujengwa jamii yenye kuaminiana na kupendana. Hii itasaidia kurejesha Tanzania iliyozoeleka machoni pa dunia.

Kushirikisha umma kutaimarisha umiliki wa mchakato na kuhakikisha kuwa suluhisho litakalopatikana inaendana na matarajio ya wengi.

Pambazuko tunahimiza kuwa ni lazima kila Mtanzania akumbuke kuwa amani ya kudumu na maendeleo yanakaribishwa zaidi kwa njia jumuishi, na siyo kufanya uamuzi wa wachache gizani.

Kuharakisha maridhiano na kuondoa dalili za uhasama kati ya vyama, umma na taasisi ni hatua muhimu mno kwa sasa ili kukomaza utaifa wetu na kurejesha staha kwa kila Mtanzania kutembea kifua mbele.

Sasa ni wakati wa kuweka maslahi ya taifa mbele, kurejesha imani kati ya wanasiasa na wananchi; watendaji na taasisi za umma na wananchi na kuunda mazingira ya utulivu yatakayowezesha Tanzania kukua kwa ustawi na maendeleo.

# Msaada...



*Wasamaria wema wakiinua bajaji iliyogongwa na gari baada ya dereva wa bajaji hiyo kulazimisha kuvuka bila kuzingatia taa za kuongozea magari eneo la Mbezi kwa Msuguri, Dar es Salaam juzi. (Na Mpigapicha Wetu)*

## Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**

**WASILIANA NA CHUMBA CHA HABARI; 0784 211 716**

*Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A – nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz*

# Dunia: Hapa na pale

## Dkt. Besigye yuko mahututi

AFYA ya kiongozi wa chama cha upinzani nchini Uganda, Dkt. Kizza Besigye ni mbaya na inaelezwa kuwa mahututi.

Taarifa iliyotolewa kwa umma na chama chake cha PFF inaeleza kuwa wiki iliyopita, baada ya maofisa wa magereza, wakiambatana na wenzao kutoka idara ya usalama walilazimika kumpeleka hospitali Besigye (pichani), huku wakijitahidi kuficha kuvuja kwa taarifa hizo.

Besigye, kiongozi ambaye amekuwa gerezani kwa muda sasa, Jumanne iliyopita alitolewa gerezani kwa siri, na kupelekwa kwenye hospitali ambayo bado serikali inaficha kuitaja, lakini baadhi ya maofisa usalama wamevujisha taarifa za kuugua kwake, bila kutaja alikopelekwa kwa matibabu.



Hata hivyo, inaaminika kuwa amelazwa kwenye hospitali moja ya serikali inayotumika kutibu viongozi.

## Mke wa Odinga 'aula'

IDA Odinga, mke wa aliyekuwa kiongozi wa upinzani nchini Kenya, Raila Odinga, ameula, baada ya Rais Willian Ruto kumpa dhamana ya kuwa kuwa Balozi wa Kenya na Mwakilishi wa Kudumu wa Shirika la Umoja wa Mataifa kuhusu Mazingira (UNEP).

Mkuu wa Utumishi wa Umma, Felix Koskei, amesema uteuzi huo unatambua huduma ya Ida Odinga kwa umma, hasa kwenye kutunza mazingira.

Koskei alieleza kuwa kazi yake ni ushahidi wa uongozi wa kujitolea, ujasiri, na dhamira ya kudumu ya kuendeleza elimu na uwezeshaji wa wanawake.

Odinga alifariki kwa ugonjwa wa moyo nchini India alikopelekwa kwa matibabu. Alikuwa kinara wa siasa za Kenya na kiungo muhimu kwa utulivu wa nchi hiyo.

## Hadhari zaidi Greenland

UJERUMANI imeungana na nchi zingine tajiri duniani kuitahadharisha Marekani juu ya uamuzi wake wa kuivamia Greenland.

Waziri wa Fedha na Naibu Chansela, Lars Klingbeil amesema kuwa uamuzi wa Marekani kuivamia Greenland hauna tofauti na uvamizi wowote unaolaaniwa na Marekani.

Amesema kuwa mbali na kukiuka sheria za dunia, hatua ya Marekani kwenda kuitawala Greenland kwa mabavu ni kuwanyima wananchi wa nchi hiyo uhuru wao, kwani uhakika ni kwamba hawakuomba kuongozwa na Marekani. Greenland ni kisiwa kikiwa sehemu ya Denmark.

## Trump ashushiwa shutuma nzito

IRAN imemshutumu Rais wa Marekani, Donald Trump na kumuita kuwa ni mhalifu asiyekuwa na tofauti na wengine wenye sifa hiyo.

Kiongozi Mkuu wa Iran, Ayatollah Ali Khamenei aliweka wazi kuwa nchi yake inaamini na kulaani kile alichokiita kuwa ni uhalifu dhidi ya dunia unaofanywa na Rais Trump. Ameshutumu Marekani kuvamia nchi zingine.

Marekani pamoja na nchi zingine zinaishutumu Iran kwa kusababisha vifo vya waandamanaji wanaotajwa kufikia 3,000, ambao walikuwa wakishambuliwa na vikosi vya usalama vya Iran wakati wa maandamano ya wananchi wake wanaowapinga kile wanachoeleza kuwa uongozi mbovu na kupanda kwa gharama za maisha.



"Tunamchukulia Rais wa Marekani, amekuwa mhalifu kama wengine ambao nchi hiyo imekuwa ikiwalaumu kwa kukiuka haki za binadamu na kuingilia uhuru wa nchi zingine," alisema Ayatollah.

Na Mzee TAI

# Huyu mbunge aache kuwa mtoto

MIMI mzee wenu nilianza mwaka huu kwa furaha, licha ya kuchukizwa na mazonge ya mwaka jana – yale ya wakati wa uchaguzi mkuu na siku chache baadaye.

Nimekaa na chuki kuu dhidi ya wote waliohusika na kadhia hiyo, lakini nafarijika kwamba sasa kuna mambo yanaendelea, huenda haki ikapatikana na wale wenye kuwajibika tutawaona baada ya haki kuwekwa hadharani.

Nawaomba tu watoto, wajukuu na Watanzania wenzangu ambao wengi tulikumbwa na janga lile tukae kwa utuo. Makalio yote yachukue nafasi yake. Kazi ya haki kupatikana inasukwa kwa ustadi mkubwa na tume, taasisi na ofisi nyingi zikiwa zimeweka miguu sawa kwa matokeo. Tusubiri.

Hata hivyo, nikiendelea kuwatia moyo, juzi nikielekea kuchukua dawa zangu za 'presha,' pale hospitali, nakumbana na picha mjongeo kwenye simu yangu ya kupangusa, niliyoletewa na mjukuu wangu Jakaya.

Katika picha ile nasikia tambo za kila aina. Ni kama kuna mzozo wa wakubwa. Nakaa sawa na kuvuta miwani yangu ili kuyapa mwanga na nguvu maozi yangu, maana yameishiwa 'pumzi' hayaoni vyema kwa uzee.

Lahaula! Namuona mjukuu wangu mmoja, huyu ni mbunge. Namuona vyema sana akirusha ngumi baada ya kuzongwa na yule jamaa anayemuita mwekezaji.

Nashangaa, huyu si anatamkwa kuwa mheshimiwa mbunge, sasa amepandwa vipi hasira hata kuvunja heshima yake, tena mbele ya makamera ya waandishi!

Yaani, mheshimiwa kaamua kuacha hadhi ya uheshimiwa. Kaamua kuwa Mandonga, yule anayejiita "Mtu Kazi." Mbona kajidhalilisha sana.

Eniwei, nikavuta kumbukumbu zangu na kugundua kuwa huyu ndiye anayeichukia elimu, kila mara akitamka kuwa wasomi ni wajinga, kwamba ndiyo wanaokwamisha maendeleo.

Nikaamini kuwa labda ujinga wake umemsukuma hata kujiita kuwa ni mhuni, ili ajiweke kwenye kundi hilo na sasa aweze kupigana mwasumbwi vyema. Nimesikitika sana.



Nikavuta vyema akili zangu, nikabaini kuwa huyo mheshimiwa aliyekosa hadhi hiyo kwa muda wa tukio lile, alikosea mambo kadhaa ya kiitifaki. Hakupaswa kuyafanya hata kama ameudhiwa na nani, tena mbele ya kamera!

Kwanza mbunge huyo mwenye chuki na elimu anapaswa kutambua kuwa katika tukio lile alivunja ama kukiuka kanuni muhimu ya kamati ya halmashauri kutembelea eneo kama lina mgogoro, kuita wahusika, kuwahoji, ikiwezekana kwenye kikao cha ndani kabla ya kutoa uamuzi. Yeye alikomalia kuwa mwekezaji asimamishe shughuli papo hapo. Ni kosa.

Ieleweke kuwa kanuni ya miongozi ya halmashauri namba 16(6), inasema; mjumbe anapozungumza ataelekeza mazungumzo yake kwa mwenyekiti, sasa sijui mwenyekiti alikuwepo au la, au mbunge mwenyewe ndiyo cheameni! Mimi sijui, mpaka niulize labda.

Zaidi sana nikamsikia anaamuru kuitwa kwa askari mmoja mkubwa wa wilaya – "hebu mwambieni OCS awepo." Hii hatari sana, sijui ndiyo mazoea ya kudogosha mhimili mwingine. Ni hatari!

Nikakumbuka kuwa mwenye mamlaka ya kuamuru, kwa mujibu wa sheria yao wenyewe Na. 7 ya Mwaka 1982 (Sura ya 287), Kifungu cha 74(4).

Hakika mambo ni mengi, wakati naendelea kumsimulia mjukuu wangu, mara nikapitiwa usingizi, kushtuka, niko hospitali tunakaribia kuondoka kwa kuwa mjukuu alikuwa amechukua dawa zangu.

Habari Kuu

# ‘Tukosoane, tusitekane, tusiuane’




*Kiongozi wa Chama cha ACT Wazalendo, Dorothy Semu, akiweka shahada la maua kwenye kaburi Edwin Mtei.*

**Na Mwandishi WETU**

MUASISI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Edwin Mtei, ameonyesha nguvu yake hata baada ya kifo.

Kifo chake kimeibua mambo makubwa kitaifa.

Kifo cha Mzee Mtei kimeibua mjadala wa kitaifa kuhusiana na mambo mbalimbali ikiwamo maridhiano, fikra huru na maridhiano.

Pia, watu maarufu, viongozi wa vyama, serikali wamekutana na kuhimiza mambo makubwa kadhaa yenye kuonyesha Watanzania wanataka nini.

Inaweza kusemwa kuwa kifo cha Mzee Mtei kimekuja wakati muafaka, kutokana na waombolezaji kutumia wasifu na tasnifu ya maisha yake kuhimiza umuhimu wa kuliponya taifa, misimamo na kufanya kazi kwa bidii.

Mzee Mtei, ambaye alikuwa gavana wa kwanza mzalendo na muasisi wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), alifariki dunia Jumatatu Januari 19 na kuzikwa juzi Jumamosi Januari 24, akihitimisha safari yake ya miaka 94 duniani.

Miongoni mwa waliopata nafasi ya kuzungumza ni pamoja Zitto Zuberi Kabwe, kiongozi mstaafu wa ACT Wazalendo ambaye alisema ujasiri wa Mtei wakati akiwa mtumishi wa serikali na hata baada ya kuondoka serikalini, ni jambo la kipekee, linalopaswa kuigwa na kuenziwa na viongozi wa sasa.

Sambamba na kauli yake hiyo, Zitto ameandika katika tanzia ambayo Pambazuko imeichapisha ndani ya kurasa zake kwamba sasa ni wakati wa Tanzania kuwa na watu wenye uhuru wa maoni bila kuogopa kutekwa, kupotezwa na hata kuuawa.

Zitto amesema ni wakati sasa kwa viongozi wakuu kuwahakikishia Watanzania usalama na uhuru wao wa kuikosoa kwa kuishauri serikali.

“Mzee Mtei na viongozi wengine waliotutangulia, waliweza kutofautiana bila kuchukiana; waliweza kuwa na misimamo tofauti bila kugombana; waliweza kuwa na mawazo tofauti bila kutekana; na waliweza kuamua tofauti bila kuuana,”ameeleza mwanasiasa huyo.

Amesema heshima ya mtu, kutotweza utu wa mtu ilikuwa tunu kubwa kwa viongozi hao, hali ambayo sasa haionekani Tanzania.

“Ni wajibu wetu kutafakari na kupita njia yetu ya kutofautiana bila kuvunjiana heshima, bila kupigana, bila kuuana, bila kutekana,” akaongeza Zitto.

**Busara za Mbowe**

Mwenyekiti (mstaafu) wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, ambaye baada ya kimya cha mwaka mmoja ametoa kauli nzito kuhusu mustakabali wa taifa ambayo nayo imezua gumzo.

Akizungumza wakati wa kutoa salamu za familia ya Mtei, Mbowe ameitaka serikali kuchukua hatua madhubuti za kurekebisha makosa ya kisiasa ambayo yamesababisha nchi kuwa “vipande vipande.”

Katika salamu hizo za familia kwenye mazishi ya hayo, Mbowe alisema sasa ni wakati muhimu kuliponya na kuliunganisha taifa.

Inaendelea Uk.7

# 'Tukosoane, tusitekane, tusiuane'

Inatoka Uk. 6

Aliilaumu serikali kwa kuwepo madai ya kuonea viongozi na wanachama wa Chadema na vyama vingine vya upinzani kwa kuwadhulumu haki zao, jambo ambalo limewafanya viongozi hao kuonekana kuwa wakaidi.

Alisema hakuna jambo la maana na muhimu kama uhuru wa watu katika nchi yao, na inasikitisha kuona viongozi wa Chadema wana maumivu, viongozi wao wamejaa magerezani bila kujali kuwa wanastahili kufaidi matunda ya nchi zao.

Alisisitiza kuwa umma unalitaka taifa liwe na furaha, lakini furaha hiyo haitapatikana iwapo wanasiasa wa upinzani wataendelea kuonewa na serikali.

Mbowe alisema historia ya maisha ya Mtei inaonyesha jinsi alivyokuwa mtu wa misimamo na ndio maana hata chama alichokiasisi kimekuwa hivyo.

"Chama hiki kinaitwa cha Demokrasia na Maendeleo kwa maana kwamba pale kwenye demokrasia ya kweli maendeleo ni inevitable (ni lazima) kuja," alisema Mbowe.

Lakini pia aliwageukia viongozi wa Chadema na kuwataka kukubaliana na hatua zitakazochukuliwa na serikali kulitibu taifa iwapo watajihakikishia kuwa hatua hizo ni za dhati, kwa kuwa anaamini kukutanishwa kwa viongozi wa Chadema na serikali katika msiba huo wa Mtei ni mpango wa Mungu.

**Askofu: Tutubu, tuzungumze**

Katika ibada hiyo ya maziko, Askofu (mstaafu) wa Kanisa la Anglikana, Simon Makundi, alisema Mtei alikuwa jasiri, alifundisha haki na uadilifu na hata alipotofautiana na Rais Mwalimu Julius Nyerere, walizungumza na walifika mahali wakakubaliana kutokubaliana, kisha wakazungumza bila haya wala unafiki katika kweli na haki na walipata uamuzi bora na kuendelea mbele.

"Binadamu hamuwezi kukubaliana kila kitu, hiyo haiwezekani, hata watoto wa baba na mama mmoja hutofautiana, lakini mkitofautiana mzungumze, bila haya wala unafiki katika kweli na haki na Mungu atawapa uamuzi bora mtaweza kuendelea..."

Inaendelea Uk 32



*Waziri Mkuu Dkt. Mwigulu Nchemba akitia saini kitabu cha maombolezo ya msiba wa aliyekuwa gavana wa kwanza wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Edwin Mtei, nyumbani kwake Tengeru, Wilaya ya Arumeru Mashariki, Arusha juzi. (Picha na OWM)*

# Chadema yalia kukandamizwa




Mwenyekiti Chadema, Tundu Lissu

**Na Mwandishi WETU**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), ambacho ni chama kikuu nchini, kinazidi kuandamwa.

Jeshi la Polisi nchini limeendelea kuwakamata viongozi wa chama hicho maeneo mbalimbali kwa tuhuma kadhaa ikiwemo uchochezi.

Wiki iliyopita, jeshi hilo lilitumia nguvu kuzuia wanachama wa Chadema kuendesha shughuli za kijamii wakati wakisherehekea miaka 33 tangu kuanzishwa kwa chama chao.

Kwa muda sasa chama hicho hakijaweza kufanya shughuli za kisiasa kutokana na amri ya mahakama, lakini kwa shughuli nyingine ambazo hazimo kwenye amri ya mahakama chama hicho kimeendelea kukosa vibali.

Hivi sasa kuna viongozi wengi wa Chadema, wakiongozwa na mwenyekiti wao wa Taifa, Tundu Lissu, ambao wako mahabusu wakikabiliwa na kesi.

Kwa upande wake, Lissu yupo mahabusu kwa takribani miezi minane sasa akikabiliwa na tuhuma za uhaini.

Katika matukio kadhaa, wanachama wa Chadema wamekamatwa na kushikiliwa na Polisi, lakini wakaachiwa bila kufikishwa mahakamani.

Inaelezwa kuwa kutokana na 'kamatakamata' hiyo, wanachama wengi wa Chadema wamejenga chuki dhidi ya Jeshi la Polisi wakiamini kuwa chombo hicho cha kulinda raia na mali zao, kinatumika kukihujumu.

Wakati jeshi hilo likishutumiwa hivyo, juzi Mkuu wa Idara ya Habari ya Chadema, Gerva Lyenda, aliiambia Pambazuko kwamba sasa 'vita dhidi ya Chadema' imehamia kwenye taasisi nyingine.

Amezituhumu kampuni mbili za simu za mikononi, Airtel na Vodacom kuwa wamewafungia namba za simu za chama hicho ambazo zinatumika kuchangisha fedha kwa ajili ya maadhimisho ya siku ya kuasisiwa kwa chama hicho.

Katika mazungumzo yake, Lyenda aliitaja namba iliyofungiwa kuwa ni 0789160733 (Airtel) inayomilikiwa na Mkurugenzi wa Mawasiliano na Uenezi wa Chadema, Brenda Rupia, na namba 0769823839 (Vodacom) inayomilikiwa na Mwenyekiti wa Baraza la Vijana Chadema (Bavicha).

Kwa mujibu wa Lyenda, namba ya Rupia imefungiwa kupokea fedha, lakini namba ya mwenyekiti wa Bavicha inapokea fedha, lakini hawezi kuzituma popote wala kuzitoa.

"Hizi ni namba za chama. Chama chetu kinazidi kupata misukosuko kila kunapokucha na hivi tunavyozungumza kampuni za simu zimezifungia namba zetu zinazotumika kuchangisha fedha kwa ajili ya shughuli za chama," anasema.

"Namba zote hizo zilifungiwa wiki iliyopita zikiwa ni siku tatu tu tangu zilipoanza kukusanya fedha na kwa upande wa hiyo namba ya Brenda, ilifungiwa ikiwa na shilingi zaidi ya milioni moja…"

"Kwa hiyo, pamoja na kwamba kulikuwa na mwitikio mzuri wa watu kuchangia fedha, kwa sasa fedha zote zinazotumwa katika namba ya Rupia zinawarudia waliozituma," amesema Lyenda.

Inaendelea Uk. 9

# Chadema yalia kukandamizwa

Inatoka Uk. 8

Kuhusu hatua zitakazochukuliwa na Chadema dhidi ya kampuni hizo, Lyenda alisema chama hakijakaa na kuamua kuchukua uamuzi wowote.

Hata hivyo, wiki iliyopita Mkurugenzi wa Sheria na Haki za Binadamu Chadema, Gaston Garubindi, alitoa taarifa kwa vyombo vya habari akiishutumu Airtel kuhusika kukidhoofisha chama chao.

Garubindi alitoa shutuma hizo kutokana na kile alichosema kampuni hiyo kufungia namba hiyo bila msingi wowote.

Katika taarifa yake hiyo kwa vyombo vya habari, Garubindi aliitaka kampuni hiyo kuifungulia laini hiyo ili wananchi waendelee kuchangia fedha kwa ajili ya maadhimisho ya siku ya kuzaliwa kwa chama chao.

"Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kinautaarifu umma kuwa, namba ya simu ya Mkurugenzi wa Mawasiliano na Uenezi wa Chadema, Brenda Rupia iliyokuwa ikitumika kuchangisha michango kwa ajili ya maadhimisho ya siku ya kuzaliwa kwa chama, imefungiwa na kampuni ya Airtel Tanzania tangu Januari 19, 2026," ameongeza.

Amesema hata baada ya kuwasilisha malalamiko yao kampuni hiyo imegoma kueleza kwa nini wameifungia namba hiyo, badala yake wamesema wanamtaka mhusika kufika katika ofisi zao popote nchini.

Aliitaka kampuni hiyo kuifungulia namba hiyo mara moja kwani hakuna sababu yoyote ya msingi ya kuifungia.

Wakati huohuo, Garubindi aliiambia Pambazuko juzi, kwamba chama kinajiandaa kutoa tamko ni hatua gani watakazozichukua dhidi ya kampuni hizo.

**Airtel wazungumza**

Mmoja wa viongozi wa ngazi za juu wa Airtel Tanzania, aliyependa kutotajwa jina, alizungumza na Pambazuko kwa simu Januari 23, mwaka huu, lakini hakutaka kukubali wala kukataa kuwapo kwa malalamiko hayo, badala yake akamuomba mwandishi wetu ampe muda wa kufuatilia suala hilo.

"Kama ni hilo, nakuomba unipe muda kidogo nilifanyie kazi maana hilo siyo jambo dogo, nitakurudia baadaye," alisema kiongozi huyo na kukata simu.

Mwandishi wetu alipompigia tena simu siku hiyohiyo, alisema hajakamilisha suala hilo na kuomba apewe muda zaidi.

"Hilo siyo jambo dogo kaka, nalifuatilia hapa, naomba unisubiri," alisema ingawa hakutoa majibu kama alivyoahidi.

Juzi Jumamosi, ofisa huyo alizungumza tena na mwandishi wetu na kusema suala hilo ameshalifikisha kwa viongozi wake wa juu wanalifanyia kazi.

"Mimi binafsi sina majibu maana suala hilo liko kwenye management, nikipata majibu nitakurudia," alisema ofisa huyo, lakini hakumrudia tena mwandishi wetu hadi gazeti lilipokwenda mtamboni.

**Vodacom wakaa kimya**

Mmoja wa wafanyakazi wa Vodacom Tanzania aliyeko katika kitengo cha habari, alipozungumza na Pambazuko, aliahidi kufuatilia suala hilo na kutoa majibu kwa mwandishi wetu, lakini hakufanya hivyo.

Wakati hayo yakiendelea, suala la Chadema kuchangisha fedha kutoka kwa wafuasi wao kupitia laini za simu, limekuwa likifanyika mara kwa mara.

Kwa mfano, mwaka 2007 Chadema kilianzisha operesheni maalum ya kukijenga chama chao iliyopewa jina la Oparesheni Sangara ambapo sehemu ya fedha za kufanikisha oparesheni hiyo, zilikuwa zikichangwa na wafuasi wao.

Mwaka 2012, Chadema kilianzisha oparesheni nyingine iliyopewa jina la Movement for Change (M4C) ambayo moja ya vyanzo vyao vya kupata fedha za kuimarisha chama chao, ilikuwa ni michango ya fedha kutoka kwa wafuasi wao walizokuwa wakizichanga kupitia simu ya mkononi.

Inaendelea Uk. 21

Tafakuri ya Bagonza



Na Dkt. Benson BAGONZA

# Nani awe mwamuzi wa haki Tanzania; fedha au mabeberu?

TUNA mambo mengi na muda hautoshi kuyasikiliza yote.

Mzee Joseph Butiku kamaliza kusema. Kapingwa na kupuuzwa, lakini tujiulize; saa mbovu ikisema muda sahihi, tutaitii na kuamka au tutapuuza?

Mzee Butiku anaweza kuwa katumwa au kachanganywa na wale jamaa, lakini jambo moja kapatia – kwamba hatuko sawa na tuna tatizo.

Shetani aletaye habari njema anaweza kuwa bora kuliko malaika aletaye habari mbaya.

Natafakari, kwamba mtu mzito (Kigogo kweli), kaniita. Kasema “tatizo ni namba moja na mbili, hawapatani, lakini namba mbili hana hela tumemkimbia. Hana lolote yule. Siasa za umaskini aliondoka nazo Kambarange. Huyu ni Yuda tu kamsaliti mwenzake”

Nikamuuliza; fedha zimeanza lini kuwa kigezo cha uongozi? Akakata simu. Wanaopenda fedha hawapendi kuulizwa maswali magumu.

Baadaye kaniita mwingine. Huyu ni kada wa chama chetu kilichogeuka chama chao. Akasema, “hata uchaguzi ukirudiwa tutashinda. Tuna hela za kutosha kununua uchaguzi mpaka 2035. Hakuna asiye na bei nchi hii. Hata wewe tunakulia timing.” Nikamwuliza hata huu uchaguzi unaobishaniwa mliununua? Akajibu kwa kifupi akasema, “kumbe wewe hujui!?”

Nikatoa kilio; “wewe fedha umelaaniwa ndiyo maana ulimuuza Yesu.”

Muda ukapita, simu ikaita, kumbe anapiga askari asiyevaa kombati isipokuwa suti. Anatoka lile “jeshi la malaika wa duniani.” Nililiamini jeshi hili mpaka nikajisahau.

Akasema, “ mkononi tuna chuma na mkwanja. Mtu achague moja. Apokee mkwanja mambo yaishe au akatae ale chuma.” Nikabaki mdomo wazi.

Zamani zetu askari wa jeshi la malaika hawa angeweza kukaa na sanduku la hela za kazi maalum,” lakini akaenda duka la Mangi kukopa chumvi. Nini kimetokea? Ni fedha zimewaharibu malaika wetu; siyo Mabeberu.

Akaja mbunge na waziri mstaafu. Akasema; “fedha ni kila kitu. Ni rahisi kumhonga mbunge apitishe sheria au bajeti kuliko kumhonga karani wa ofisi akuibie nyaraka. Lunch ya Ikulu na semina moja yenye posho kubwa inatosha kumlainisha. Mbunge aliyeshindikana anapewa safari moja ya nje, akirudi anagonga meza mpaka inatoboka”.

Hatuhitaji mabeberu kulivuruga bunge. Fedha inatosha na ina nguvu kuliko bunge lenyewe. Chanjo ya uzalendo kwa wabunge itoke wapi?

Nikiwa bado namtafakari huyu mbunge, mara simu ya Mnikulu inaita, akasema, “tuna ombwe (vaccum). Tiketi haielewani. Mmoja yuko tayari yaishe, lakini waondoke wote ili kuunganisha taifa. Mwingine hataki, na hela hataki. Tunajiandaa kurudi kuliokoa taifa. Hatutagusa vyombo vyetu.”

Mpaka hapa, nani asiyeona haja ya maridhiano? Wengi tunayataka. Tunachoogopa ni hila.

**Hila zinachelewesha maridhiano.**

Katika awamu ya pili, Baba wa Taifa aliandika maneno haya; “Majuto ni mjukuu, huja baadaye. Tunaweza kufikishwa mahali tukiulinganisha uongozi wa Rais Mwinyi na wa rais wa kesho tukaona kuwa chini ya Ndugu Mwinyi, pamoja na udhaifu wake wote, tulikuwa peponi” (ukurasa 52, Uongozi Wetu...).

Wajaluo wanasema; “Maskini akitabiri ujio wa nzige, huzodolewa kuwa ana hamu ya kuwala.”

***Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.***



Na Dkt. Hellen Kijo BISIMBA

## Buriani Ediwn Mtei:

# Nyota ya mwanauchumi, mwanamageuzi iliyozima

KWA masikitiko makubwa nimepokea taarifa ya kifo cha Mzee Edwin Mtei aliyekuwa Gavana wa kwanza wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na mmoja wa waanzilishi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

Mzee Mtei ameishi miaka yake 92 ya kukumbukwa. Alikuwa ni mtu aliyethubutu kusimama na kanuni hata kwa gharama ya kupoteza cheo kikubwa.

Alizaliwa Marangu, Kilimanjaro Julai 12, 1932 na kulelewa na mama yake na kufanikiwa kupata elimu bora kufikia kuhitimu Shahada ya Kwanza huko Makerere, Uganda, chuo kikuu maarufu Afrika Mashariki na duniani.

Aliporejea nchini kutoka masomoni alifanya kazi katika utumishi wa umma, kama alivyoteuliwa kuwa katibu mkuu wa Hazina na hatimaye kupewa kazi nzito ya kuwa gavana wa kwanza wa BoT ilipoanzishwa mwaka 1966 akiwa na umri wa miaka 34, ambapo alitumikia nafasi hiyo kuanzia mwaka 1966 hadi 1974.

Alipewa nafasi ya kuwa waziri wa fedha mwaka 1977 hadi 1981 alipoamua kujiuzulu.

Akiwa waziri wa fedha alikuwa mshauri wa rais katika masuala ya kiuchumi na fedha wakati huo rais akiwa ni Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Msukumo wa kimageuzi ulionyeshwa na Mtei pale alipotofautiana na Mwalimu Nyerere kuhusu mwelekeo wa sera na uchumi.

Mzee Mtei amepata heshima kwa jinsi alivyosimamia msimamo wake wa kitaaluma katika suala lililokuwa likijadiliwa kisiasa na kiongozi wake.

Mzee Mtei hakuwa mtu wa hivi-hivi, alikuwa ni mtu wa misimamo na mwenye uwezo wa kujenga hoja kwelikweli, hakuyumba au kumuogopa kiongozi wake, kwa kile alichokiamini.

Alipoona ameshindwa kuelewana na Mwalimu Nyerere, hakuamua kufanya kazi tu shingo upande, bali aliona vyema ajiuzulu kuonyesha msimamo.

Hili siyo jambo rahisi na siyo kawaida kwa watu wengi, hasa hapa nchini kwetu, ambapo kwa sasa tunaona watu wanajitahidi sana kwenda na upepo wa viongozi wao hata kama wanatambua hawako sahihi.

Ni kutokana na kujipendekeza, sasa pamezuka msemo mpya nchini wa 'Chawacracy,' unaomaanisha upevu wa kujipendekeza.

Tunampa heko Mzee Mtei kwa huo ujasiri ambao ni fundisho kwa kizazi cha sasa, kwani hata baada ya hapo aliendelea kuishi, akifanya mambo aliyoyapenda ikiwamo kilimo na shughuli zingine.

Baada ya hapo alifikia hatua ya kupata nafasi kubwa kimataifa kwenye Shirika la Fedha Duniani (IMF) akiwakilisha nchi za kiafrika katika ngazi ya kimataifa.

Kumbukumbu nyingine kubwa kwa Mzee Mtei ni pale alivyoweza kuingia katika wimbi la mageuzi wakati mfumo wa vyama vingi vya siasa unaanzishwa upya nchini na yeye kuweza kushiriki katika kuanzisha Chadema, akiwa kiongozi wake mkuu wa kwanza.

Kama tunavyofahamu chama hicho kimekua kiasi cha kuwa chama kikuu cha upinzani na hata kwa kiasi kikubwa kubadili muelekeo wa siasa hapa nchini.

Kwa buriani hii, tunakumbuka ujasiri wa kusimamia kanuni, ujenzi wa demokrasia ya vyama vingi na tumejifunza kwamba mageuzi huanza na mtu mmoja mwenye msimamo.

Ninawapa pole watoto wa marehemu, ndugu na Watanzania wote walioguswa na msiba huu mkubwa.

***Ndugu Mtei Apumzike kwa Amani.***

***Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwanaharakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.***

Habari



# Bandari ya D'Salaam kitovu uchumi DRC

**Na Mwandishi WETU**

HISTORIA ya maendeleo ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), kila inapoandikwa, lazima mchango wa Bandari ya Dar es Salaam, uonekane.

Sababu kubwa ya bandari hiyo kutajwa na kupigiwa chapuo na DRC, ni kuwa njia ya kupokea na kusafirisha shehena za nchi hiyo; iwe bidhaa za biashara, mizigo ya kuchochea uhai na ustawi wa wananchi wake, ikiwamo dawa na shehena zingine.

Bandari ya Dar es Salaam imekuwa ni rafiki mkubwa na ustawi wa DRC na kuwa chaguo lake la kwanza kupitisha shehena zake kwa kuwa upo umbali mfupi kutoka nchi hiyo hadi Dar es Salaam. Ni kilomita 3753.

Kutoka DRC hadi bandari zingine, kuna kilomita zaidi ya 5000, hivyo endapo zingetumika bandari hizo, hasa Mombasa, gharama za kusafirisha shehena zingeongezeka.

Mbali na umbali, DRC pia inaelezwa kuzingatia suala la ufanisi, utendaji wa kisasa wa vifaa na uaminifu wa wafanyakazi wa bandari za Tanzania, hasa baada ya mifumo ya fedha na ufuatiliaji wa mizigo kuboreshwa.

Msemaji Mkuu wa Serikali ya Tanzania, Gerson Msigwa hivi karibuni alitembelea Bandari ya Dar es Salaam na kueleza kuwa DRC ndiyo kinara wa kutumia bandari hiyo kwa kusafirisha na kupokea.

Inaendelea Uk. 13

# Bandari ya Dar kitovu...

Inatoka Uk. 12

"Nchi ya DRC pekee katika mwaka wa 2024/2025 imepitisha shehena kwenye bandari zetu yenye zaidi ya tani milioni 5.9, sehemu kubwa ikipita Dar es Salaam, hiki ni kiasi kikubwa ambacho haijawahi kutokea na hiyo yote ni kutokana na kuboresha miundombinu yetu mbalimbali ya ndani na nje ya bandari", alisema Msigwa.

Uamuzi wa Rais Samia Suluhu Hassan kuimarisha zaidi uhusiano na DRC, kumewezesha pia Tanzania kutenga eneo maalumu lenye ukubwa wa hekta 45 katika Bandari Kavu ya Kwala kwa ajili ya kuhifadhi shehena za DRC.

Hatua hii pia imeongeza ari kwa wafanyabiashara wa DRC na serikali yao kuendelea kutumia bandari za Tanzania kwani wanaona usalama wa bidhaa zao ni mkubwa ikilinganisha na nchi nyingine zenye bahari.

Machi 19,2025 baadhi ya "wakubwa" kutoka nchini DRC na Burundi walitembelea Bandari Kavu ya Kwala na kuona maboresho makubwa ya miundombinu na kuridhishwa, huku wakieleza kuwa "sasa malalamiko ya wafanyabiashara kutoka DRC na Burundi hayatakuwepo."

Ujumbe huo uliongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi kutoka Burundi, Christine Niragira na Mwakilishi wa Wizara ya Uchukuzi ya DRC, Roger Te- Biasu.

"Tunaipongeza Serikali ya Tanzania na tunampongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri inayofanyika hapa Kwala na kwa kutupatia eneo hili kwani ni njia ya kurahisisha ufanyaji biashara kati ya Tanzania na Burundi nasi kwa sasa tunaendelea kuliendeleza eneo hili haraka," alisema Roger Te- Biasu.

### Bandari chanzo cha mapato

Kuboreshwa kwa miundombinu na mifumo, uongozi imara wa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Plasduce Mbossa, kumewezesha sekta ya bandari kuongeza mchango wake kwenye ustawi wa Tanzania na watu wake.

Katika kipindi cha mwaka mmoja wa fedha' 2024-2025, TPA imeweza kuchangia gawio la asilimia 15 ya mapato yake ghafi kwa serikali na kuibuka kinara kati ya mashirika yote ya umma na taasisi zote za serikali.

TPA ilichangia gawio la shilingi bilioni 181.5 kutoka shilingi bilioni 153.917 mwaka 2024.

### Sababu zingine

Ukiacha Bandari ya Dar es Salaam kuwa kinara wa kukusanya na kuchagia mapato ya serikali, pia bandari zingine zimeendelea kuwa chaguo la kwanza kwa wafanyabiashara wa ndani na nchi jirani.

Mbali na maboresho, ufanisi na utendaji unaotajwa kuwa shirikishi; wafanyabiashara na watendaji wa TPA, wameendelea kufanya kazi pamoja na kutatua changamoto za haraka pindi zinapotokea.

Tanzania imebarikiwa kuwa na pwani ndefu kutoka eneo la kaskazini ambako kuna Bandari ya Tanga mpaka kusini ambapo kuna Bandari ya Mtwara ambayo inapakana na Msumbiji, pwani hiyo yote ina urefu wa kilomita 1424.


Katika eneo hilo kuna bandari za Tanga, Dar es Salaam, Bagamoyo na Mtwara. Hizo zote hutumika kwa ajili ya kuingiza na kutoa mizigo.

Bandari hizo zimekuwa na tija kwa Tanzania na hata kwa nchi zote zinazoizunguka, kwani hutumia kwa ajili ya kusafirisha bidhaa zao kwenda na kutoka ughaibuni. Nchi hizo ni Uganda, Rwanda, Burundi, Malawi na Zimbabwe.

Nchi nyingine zinazojinufaisha kwa kutumia bandari za Tanzania ni pamoja na DRC, Zambia, na Zimbabwe.



*Mkurugenzi wa TPA, Plasduce Mbossa*



Buriani

# Edwin Mtei: Ni zaidi ya nyadhifa, siasa



Na Ansbert NGURUMO

HISTORIA ya Tanzania haiwezi kusimuliwa kwa uaminifu bila kutaja jina la Edwin Isaac Mbiliewi Mtei.

Siyo kwa sababu tu alikuwa Gavana wa kwanza wa Benki Kuu ya Tanzania, wala kwa kuwa aliwahi kuwa Waziri wa Fedha, Mkurugenzi wa IMF, Katibu Mkuu wa Jumuia ya Afrika Mashariki, au kwa sababu alianzisha Chadema. Hapana.

Edwin Mtei, ambaye ameaga dunia usiku wa kuamkia Januari 20, 2026, alikuwa zaidi ya nyadhifa. Alikuwa wazo. Alikuwa na msimamo. Alikuwa taasisi inayotembea.

Kwa wengi wa kizazi cha leo, hasa vijana wanaoishi na kupigania Chadema kama ngome ya matumaini ya mabadiliko, jina la Edwin Mtei linaweza kuonekana kama kumbukumbu ya mbali, au jina linalopita haraka katika vitabu vya historia ya siasa.

Ni kwa sababu alipokuwa anafanya yote haya, wengi wao hawakuwa wamezaliwa au walikuwa watoto wadogo. Wale ambao hawajibidishi kusaka taarifa na maarifa, wanaweza wasimfahamu kwa sababu hawakumwona.

Lakini kwa hakika, kuingia kwa Edwin Mtei katika siasa za ushindani nchini Tanzania, kuliongeza chachu ambayo bila hiyo zingekuwa na taswira tofauti kabisa.

Hata Chadema aliyoasisi, kama isingefuata misingi ya Mtei, labda ingeishia vilikoishia vyama vingine vilivyoasisiwa wakati mmoja na Chadema miaka 33 iliyopita.

Mtei hakuwa mwanasiasa wa 'makelele.' Hakuwa mtafuta umaarufu. Hakuwa mpenda madaraka. Hakuwa na hila wala visasi. Alikuwa mjenzi wa misingi.

Watu wa misingi mara nyingi hawashangiliwi sana wakati wa uhai wao; hutambulika kikamilifu baada ya muda kupita.

Kutoka mchunga mbuzi hadi mtumishi wa taifa

Safari ya Edwin Mtei ilianzia mbali na meza za uamuzi wa dunia. Ilianzia Marangu, mkoani Kilimanjaro, akiwa mtoto kutoka kaya maskini aliyekuwa akichunga mbuzi.

Hapo ndipo simulizi yake maarufu iliyozaa kitabu "From Goatherd to Governor" ilipoanzia - siyo kama hadithi ya kujisifu, bali kama ushahidi kwamba nidhamu, elimu, na maadili vinaweza kumbeba mtu kutoka pembezoni mwa jamii hadi katikati ya historia ya taifa.

Alikuwa msomi aliyepitia mifumo mbalimbali ya elimu, akajijenga kwa maarifa na nidhamu kali ya kitaaluma.

Utaalamu wake wa uchumi haukuwa wa vitabuni pekee, ulikuwa wa kuelewa uhalisia wa jamii, uwezo na mipaka ya dola, na hatari za mifumo ya kiuchumi isiyozingatia mazingira halisi ya watu.

Inaendelea Uk. 15

# Edwin Mtei:

Inatoka Uk. 14

**Alithamini misingi kuliko vyeo**

Akiwa gavana wa kwanza wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Mtei aliasisi misingi ya taasisi ambayo hadi leo bado inategemewa kama nguzo ya uthabiti wa kifedha wa taifa.

Akiwa Waziri wa Fedha wa Tanzania, alionyesha mfano adimu wa uongozi wa maadili pale alipojiuzulu wadhifa wake mara tu alipohisi misingi ya utumishi wa umma inavunjwa. Katika siasa za Afrika, huo ulikuwa (na bado ni) uamuzi wa nadra sana.

Katika Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na taasisi za kimataifa, Mtei hakuwa mwakilishi wa maslahi binafsi, bali sauti ya nchi masikini zinazotafuta heshima, haki, na nafasi ya kujadiliana kwa usawa katika mfumo wa uchumi wa dunia usiokuwa sawa.

Popote alipohudumu, aliondoka akiwa ameacha mfumo, siyo kumbukumbu ya jina tu.

**Kuzaliwa kwa Chadema**

Katika kitabu chake, Mtei anaeleza wazi muktadha wa kisiasa uliosababisha kuzaliwa kwa Chadema.

Mwanzoni mwa miaka ya 1990, Rais Ali Hassan Mwinyi alimtea kuongoza Tume ya Rais ya Mapato ya Serikali, Kodi na Matumizi. Wakati huohuo, taifa lilikuwa linajadili kwa kina mapendekezo ya Tume ya Jaji Francis Nyalali kuhusu mfumo wa chama kimoja.

Mtei anaandika kwamba katika mjadala huo wa kitaifa, vikundi mbalimbali vilianza kujitokeza vikijadili uwezekano wa kuanzisha vyama vya siasa.

Baadhi ya watu waliomfahamu, waliojua misimamo yake ya kitaifa na waliodhani wangeweza kukubaliana naye, walianza kumtembelea na kuzungumza naye kuhusu wazo la kuanzisha chama kipya.

Hapo ndipo kundi la awali likaundwa, likamwomba awe mwenyekiti wake, na kazi ikaanza rasmi; kuandaa madhumuni, misimamo ya kiitikadi, na rasimu ya katiba ya chama.

Watu walifahamu misimamo yake, uadilifu wake, na fikra zake za kitaifa walimfuata - siyo kwa jazba, bali kwa matumaini ya kujenga mbadala wa kisiasa wenye fikra.

Hapo ndipo Chadema ilipozaliwa, siyo kama chama cha malalamiko, bali tanuri la mawazo mapya. Mtei na wenzake waliamini kuwa ujamaa wa kinadharia uliokuwa sugu (wa Julius Nyerere) usingeweza tena kujibu changamoto za Tanzania.

Walipendekeza uchumi unaoruhusu soko kufanya kazi, serikali kudhibiti kwa busara, kulinda maslahi ya umma, na kutoa upendeleo wa kimkakati kwa wazawa (Uzawa).

Inaendelea Uk. 16



*Maaskofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) wakishiriki ibada ya mazishi ya Edwin Mtei.*

# Edwin Mtei:

Inatoka Uk. 15

Hii ilikuwa Chadema ya awali; ya kihafidhina kitaaluma, ya nidhamu, na ya kujenga taasisi imara itakayokuwa mbadala wa CCM; Chadema yenye fikra mpya, mawazo mapya, mikakati mipya, na matumaini mapya.

### Ujasiri wa kuanza chini ya ufuatiliaji

Majadiliano ya awali yalifanyika katika British Legion Club, Dar es Salaam, kisha yakahamia katika chumba cha hoteli alichokuwa anatumia Mtei, na baadaye nyumbani kwa Kanali Geoffrey Marealle, ambaye alimkarimu pia kwa makazi. Baadaye, Freeman Mbowe alitoa Mbowe Hotel kuwa kituo cha kudumu cha vikao vya kuasisi Chadema.

Anaeleza bila jazba kwamba walikuwa wakifanya mambo yao kwa uwazi, wakifuata sheria na katiba. Hata hivyo, hilo halikuzuia vyombo vya usalama kuwafuatilia na kuwachunguza kwa karibu.

Walifahamu kuwa Idara ya Usalama wa Taifa ilikuwa inarekodi waliomtembelea nyumbani kwake Arusha, hotelini au ofisini Dar es Salaam. Lakini ufuatiliaji huo haukuwavunja moyo.

Kwa msaada wa waasisi wenza; Edward Barongo, Mustafa Simba, Brown Ngwilulupi, Shariff A. H. Selemani, Kanali Geoffrey Marealle, Bob Nyanga Makani, Freeman Aikaeli Mbowe, Mary Kabigi, Kassim Mfinanga, Costa Shinganya, Philemon Ndesamburo, Dkt. Medard Mutungi, Victor Kimesera, pamoja na wengine wengi waliotajwa katika kumbukumbu mbalimbali za waasisi, Chadema ilikusanya wanachama, ikatimiza masharti ya kisheria, na Januari 23, 1993, kwa mujibu wa kumbukumbu za Mzee Mtei, ikakabidhiwa cheti cha usajili wa kudumu.



Mwanzilishi wa Chadema, Edwin Mtei

Agosti 1993, Edwin Mtei akachaguliwa kuwa mwenyekiti wa taifa wa kwanza wa chama hicho.

### Mtei mlezi wa vizazi vya viongozi

Urathi wa Edwin Mtei hauishii Chadema. Amekuwa na ushawishi ndani ya CCM, Chadema aliyoiasisi, na vyama vingine ambavyo baadaye vilijengwa au viliimarishwa na wanachama waliohamia kutoka Chadema.

Wanachama wengi wa Chadema waliohamia CCM, ACT-Wazalendo, Chaumma na vingine, ni sehemu ya viongozi, wanaharakati, na wasomi waliopitia au kuguswa na shule ya kisiasa ndani ya chama kilichoasisiwa na Mtei.

Chama alichoanzisha kimekuwa kiota cha kulea viongozi, wengine wakabaki, wengine wakahama, lakini wote wakibeba chembe za misingi aliyoweka: nidhamu, hoja, taasisi, na heshima kwa kanuni.

### Zaidi ya mwanasiasa

Edwin Mtei alikuwa zaidi ya mchumi. Zaidi ya mwanasiasa. Zaidi ya kiongozi wa chama. Alikuwa dhamiri ya taasisi.

Alikuwa mtu aliyethamini utulivu kuliko makelele, misingi kuliko umaarufu, na historia idumuyo kuliko papara na mihemko ya muda mfupi.

Alipanda mbegu za demokrasia bila kujua ni nani atavuna kivuli chake. Aliacha Chadema ikiwa taasisi inayojijenga taratibu na kuimarika licha ya changamoto lukuki kutoka kwa dola.

Aliacha mfano wa mtumishi wa umma anayejua wakati wa kushika madaraka na wakati wa kuyaacha.


Alianza akiwa mchunga mbuzi. Akawa msomi aliyebobea katika masuala ya uchumi na kodi. Akawa mtumishi wa taifa. Akajenga taasisi. Akapanda mbegu. Akaiwacha ikue.

Huo ndio urithi na urathi wa Edwin Mtei.

Na Chadema, pamoja na taifa kwa ujumla, ina wajibu wa kumuenzi siyo kwa maneno pekee, bali kwa kuishi misingi ya demokrasia, uadilifu, na fikra pana alizozisimamia kwa maisha yake yote.

*Mwandishi wa makala haya ya buriani ni Rais wa SK Media, taasisi ya habari inayoandaa mafunzo, machapisho na miradi.*

# Bima ya Afya kwa Wote kuanza leo



Waziri wa Afya, Mohamed Mchengerwa

**Na Mwandishi WETU**

SERIKALI imetangaza rasmi kuanza utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mpango wa Bima ya Afya kwa Wote kwa kundi la wananchi wasio na uwezo linalohusisha wazee, watoto, wajawazito na walemavu.

Tangazo lililotolewa na serikali mwishoni mwa wiki iliyopita likibainisha kuwa watu katika kundi hilo watagharamiwa na serikali moja kwa moja.

Aidha, serikali imetangaza kwa makundi mengine yatakayojilipia, kitita cha chini kabisa kitakuwa na gharama ya shilingi 150,000 itakayohusisha kaya ya watu wasiozidi sita.

Hayo yamebainishwa Ijumaa iliyopita jijini Dodoma na Waziri wa Afya, Mohamed Mchengerwa, kwenye kikao cha kujadili utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote na viongozi na watendaji ngazi ya mikoa, wilaya pamoja na Serikali za Mitaa.

Waziri Mchengerwa amesema Bima ya Afya kwa Wote itaanza leo Januari 26, 2026 na kuwataka watendaji kuhakikisha wananchi wanapata elimu kabla ya kujiunga.

Aidha, amesisitiza kuwa vituo vya kutolea huduma vinapaswa kutoa huduma bora za afya kwa wananchi watakaojiunga na mpango huo.

Alisema haitakuwa na maana kwa kaya kulipa shilingi 150,000 halafu wakakosa huduma au kupata huduma zisizo bora.

Waziri Mchengerwa amesema kuwa kwa gharama ya shilingi 150,000 watu sita walio kwenye kaya moja, akiwamo mchangiaji, mwenza wake na wategemezi wanne watakuwa na haki ya kupata huduma za afya kwenye vituo vilivyoainishwa bila ya kutakiwa kuongeza malipo mengine.

"Wategemezi hao wanne wanaweza kuwa ni mzazi wa mwanachama au mzazi wa mwenza wa mwanachama, mtoto wa mwanachama wa kuzaa, kuasili au wa kambo aliye na umri chini ya miaka 21 au ndugu wa damu wa mwanachama aliye na umri wa chini ya miaka 21," amefafanua Waziri Mchengerwa.

Amesema chini ya utaratibu huo, kitita cha huduma muhimu kitatolewa kwa kuzingatia utaratibu wa rufaa katika vituo vya kutolea huduma za afya vitakavyoingia mkataba na skimu za Bima ya Afya.

Ili kufikia azma ya uhakika wa matibabu kwa wananchi wote kupitia Bima ya Afya, Mchengerwa akasema viongozi na watendaji hawana budi kuhakikisha kuwa elimu sahihi inawafikia wananchi waweze kujua umuhimu wa kuwa na Bima ya Afya na pia haki zao watakapojiunga na mpango huo.

"Mafanikio, mapungufu na changamoto za utekelezaji zitatathiminiwa kupitia uongozi wa Mkoa husika. Mkoa ambao wananchi wake wanaelewa mfumo, wamesajiliwa kwa wingi na wanapata huduma bila vikwazo, utaonekana kama mfano wa uongozi unaotekeleza maamuzi ya serikali kwa ufanisi," alisema.

Kwa mujibu wa Mchengerwa, hatua hii ya serikali inamaanisha kuwa ajenda ya Bima ya Afya kwa Wote ni lazima iondoke kwenye ngazi ya waraka na iingie kwenye utekelezaji kuanzia leo huku ikiwa ni ajenda ya kila siku ya uongozi wa Mkoa.

# Mavunde awashukia wanaohodhi leseni


Waziri wa Madini, Anthony Mavunde

Na Mwandishi WETU

SERIKALI imetoa onyo kali kwa wafanyabiashara waliochukua leseni za utafutaji wa madini na kukaa nazo muda mrefu bila kuzitumia kuendeleza maeneo waliyomilikishwa.

Akizungumza jijini Dodoma wiki iliyopita, Waziri wa Madini, Anthony Mavunde aliwaagiza maofisa madini nchini kote kupeleka ofisini kwake taarifa kuhusiana na leseni za aina hiyo ndani ya kipindi cha wiki moja.

Akaahidi kuwa pindi akipata taarifa hizo, kazi yake itakuwa ni kuzifuta leseni hizo.

Mavunde ametoa agizo hilo akisema inasikitisha kuwa baadhi ya watu wamechukua leseni hizo na kumilikishwa maeneo yenye madini na kuyaacha bila kuyafanyia kazi huku mamilioni ya wachimbaji wadogo wakihangaika kutafuta maeneo ya kufanya shughuli zao.

Agizo hilo la Mavunde linaashiria mabadiliko makubwa ambayo serikali inataka kuyafanya kuelekea utekelezaji wa sheria na sheria za madini.

Wachambuzi wa masuala ya uchumi wanasema hatua hiyo inalenga kufungua uwekezaji, kuharakisha maendeleo ya rasilimali za madini na kudhibiti vitendo vya kuhifadhi haki za madini kwa nia ya ubashiri.

Mavunde anasema wizara imebaini kuwa kuna baadhi ya wafanyabiashara ambao wamepewa leseni hizo, lakini hawana mpango wa kuyaendeleza maeneo waliyomilikishwa.

"Wamehodhi leseni huku wakitafuta wawekezaji ili wawauzie maeneo hayo kwa kutumia leseni tulizowapa. Hilo halikubaliki. Tunao watu wengi ambao wapo tayari kuyaendeleza maeneo hayo kwa kuchimba, tutawanyang'anya waliohodhi leseni na kuwapa watu hao," alisisitiza.

Mavunde alitoa agizo hilo wakati wa kikao cha tathmini ya utendaji kazi na viongozi wakuu wa Wizara ya Madini, ambapo aliagiza kufanyika mara moja kwa ukaguzi wa kitaifa wa wamiliki wote wa leseni za utafiti.

Kwa mujibu wa mfumo wa sheria za madini Tanzania, leseni za utafiti hutolewa zikiwa na masharti ya wazi, ikiwemo utekelezaji wa programu za utafiti ndani ya muda uliobainishwa, matumizi ya fedha kama ilivyopangwa, pamoja na uwasilishaji wa taarifa za mara kwa mara.

Hata hivyo, Mavunde anasema wizara imebaini kuwa baadhi ya wamiliki wa leseni wameshindwa kufanya shughuli zozote za utafiti, badala yake wakishikilia maeneo makubwa yenye utajiri wa madini wakisubiri kupata wawekezaji.

**Sera inasemaje?**

Hatua inayochukuliwa na wizara inaakisi mwelekeo mpana wa mageuzi ya sekta ya madini nchini, ikiwa ni muendelezo wa hatua kama hizo katika kipindi cha miaka ya hivi karibuni.

Chini ya matakwa ya sera ya madini, mkazo umewekwa kutoka utoaji wa leseni pekee kwenda kwenye kuongeza thamani, uzingatiaji wa sheria na uwajibikaji.

Hivyo, wawekezaji ambao wanachukua leseni hizo na kuacha kuzifanyia kazi wanakwenda kinyume na sera hiyo.

Sekta ya madini inachangia kwa kiasi kikubwa uchumi, ikichangia takribani asilimia 10 ya Pato la Taifa (GDP), zaidi ya asilimia 50 ya mapato ya mauzo ya nje, pamoja na mapato mengine ya serikali kupitia shughuli zinazofanywa sambamba na sekta ya madini.

Dhahabu bado ni madini makuu, lakini pia Tanzania inaendelea kujipanga kimkakati katika madini muhimu kama graphite, nickel, na madini adimu (rare earth elements).

Maofisa wa serikali wanasema wafanyabiashara wanaohodhi leseni wanavuruga malengo haya kwa kufunga maeneo yenye fursa kubwa ambayo yangeweza kuvutia wawekezaji makini wenye uwezo wa kiteknolojia na kifedha.

# Bei ya vyakula kuendelea kupanda Iringa Mjini

**Na Idd UPETE**

WAFANYABIASHARA wa viazi mviringo na vitunguu katika Soko Kuu la Manispaa ya Iringa wametahadharisha kuwa bei ya mazao hayo, itaendelea kupanda kwani hali ya hewa na mvua siyo rafiki kwa mazao hayo.

Wakizungumza na Pambazuko wamesema kwa sasa inaonekana kuwa mambo yako shwari, kwani upatikanaji wa mazao hayo kutoka kwa wakulima wa maeneo mbalimbali ya nchi uko vizuri na usambazaji siyo shida kwa sababu barabara za vijijini zinapitika.

Emmanuel Sanga, mfanyabiashara wa viazi mviringo anasema hivi sasa gunia la ujazo wa kilogramu 100 kutoka mkoani Njombe linauzwa shilingi 65, 000 huku viazi vya kutoka wilayani Kilolo, Iringa kwa uzito huo huo likiuzwa shilingi 55,000.

Alisema bei inatofautiana kwa sababu viazi vya Kilolo vinaoza mapema.

"Kwa wakulima wakubwa wa Njombe na Kilolo, unaweza kupata kwa bei ya jumla ambayo ni himilivu, tofauti na wakulima wadogo ambao hawana hofu sana ya kuharibika kwa zao hilo likiwa shambani kwani wanunuzi kwao siyo haba,"alifafanua.

Alisema kuwa wao wakiwa wafanyabiashara kwa sasa wanaagiza viazi kulingana na mahitaji ya wateja wao ambao ni wa kudumu.

Lakini alionya kuwa ifikapo Februari, mwaka huu, hali inaweza kubadilika kwani viazi kutoka Mufindi, Mbeya na Dabaga "vitakata" na hivyo kutegemea zaidi kutoka mkoani Njombe ambako uzalishaji wake ni wa mwaka mzima.

Hivyo, kuna uwezekano mkubwa kuwa kuanzia mwezi ujao bei ya mazao hayo ikaongezeka kutokana na kupungua kwa uzalishaji.

"Kama wafanyabiashara hawatapandisha bei, basi watapunguza kipimo. Kwa mlaji utagundua kuwa sokoni kuna mabadiliko ya bei pale utakapoagiza chips na kukuta sahani haijai au umepewa ndogo," anafafanua Sanga.

Hivi sasa bei ya rejareja kwa debe la viazi la kilo 20 ni shilingi 15,000.

Kwa upande wa vitunguu, Kelvin Mkini, mfanyabiashara wa jumla ambaye pia analima zao hilo, alisema kuwa kwa sasa gunia moja la kilogramu 100 linauzwa shilingi 100,000 huku akitabiri kuwa ifikapo Machi, bei inaweza kupanda hadi kufikia shilingi 150,000. Kwa rejareja debe la vitunguu la kilo 20 linauzwa shilingi 20,000.

Vitunguu vingi sokoni hapo vinatoka maeneo ya vijiji vya Iringa ambavyo ni pamoja na Tanangozi, Kiwele, Ismani, Idodi, Ilula, Pawaga, Dabaga na kiasi kidogo kutoka Igawa mkoani Mbeya.


"Changamoto ya vitunguu ni aina ya mbegu na uhifadhi, kama ukipata mbegu duni inaoza mapema na kama huna chumba au ghala la kuhifadhia vitunguu vinachukua muda mfupi sana kuoza," alisema Mkini.





Tanzia

# Hamba kahle Gavana Edwin Mtei




Na Zitto KABWE

TURUDI Desemba 1979, wewe ni Waziri wa Fedha. Umepeleka wageni kwa rais. Rais mwenyewe ni Julius Nyerere. Rais hawataki wageni hao ila wewe unaona ni wageni muhimu kulingana na hali ya uchumi wa nchi wakati huo.

Unajua hali ya nchi maana umekuwa gavana mwanzilishi wa Benki Kuu ya Tanzania, Katibu Mkuu wa Jumuia ya Afrika Mashariki ambayo imevunjika punde na sasa Waziri wa Fedha.

Rais amegoma, amekasirika na wewe umeondoka na wageni wako nyumbani kwa rais ukiwa umekasirika.

Yaani wewe waziri wa fedha umefura kwa hasira na amiri jeshi mkuu wako naye amevimba kwa hasira.

Umerudi ofisini kwako. Waziri mwenzako, kilimo, anakuletea ujumbe kuwa mwende kwa rais, huyohuyo Julius, kuhusu kununua shamba.

Unajua hazina haina kitu kiasi cha kupata shida kulipa mishahara. Unakwenda kwa rais unamkatalia hilo atakalo yeye na huyo waziri mwenzako.

Umekasirika zaidi. Unarudi ofisini, unaandika barua ya kujizulu unatoka kumpelekea rais unakutana na msaidizi wa rais anakuletea barua kutoka kwa rais. Huisomi ila unakimbia kwenda kwa rais kumpa barua yako.

Rais anakuuliza, umepata barua yangu? Unasema ndio, lakini hujaisoma. Unampa yako. Anakubali barua yako.

Rais anaagiza barua yako ndio iwe rekodi rasmi ya umma. Umejiuzulu badala ya kufukuzwa.

Nchi nzima yanaandaliwa maandamano, hatutageuka jiwe la chumvi. Maandamano yanapingana na mawazo yako. Unaonekana adui wa taifa. Punde rais huyohuyo anakupeleka nje kuwa mwakilishi wa Afrika katika Shirika la Fedha la Kimataifa. Shirika ambalo wageni wake walikataliwa.

Huyu ndiye Edwin Mtei. Hiyo ndio Tanzania. Huo ndio ukomavu ambao taifa letu lilikuwa limefikia miaka 20 tu baada ya Uhuru.

Kwamba mnaweza kupishana mawazo bila kuwekeana chuki na mkaendelea kuheshimiana. Ni ukomavu huu ambao uliliweka taifa pamoja. Ni ukomavu huu ambao sasa, miaka 60 baada ya uhuru haupo na taifa lipo kwenye mtanziko mkubwa.

Huu ndio msingi pia ambao Mzee Edwin Mtei aliujenga hata alipoanzisha pamoja na wenzake Chama cha Chadema. Kwamba zifanywe siasa kwa kupingana bila kupigana, bila kujenga chuki na unaona mawazo yake haya kwenye kitabu chake – 'kutoka mchunga mbuzi mpaka gavana.'

Leo tunamuaga Gavana Mtei. Anaenda kuungana na Nyerere. Anaenda kuonana na rafiki zake kina Bob Makani, Victor Kimesera, Brown Ngwilulupi, Mama Mary Kabigi na wenzake wengi.

Maisha ya Edwin Mtei ni duara lilikamilika. Aliyaishi kwa ukamilifu wake. Hakika tunapaswa kusherehekea maisha yake. Tunapaswa kuyatafakari mapito yake.

Gavana Mwanzilishi wa Benki Kuu ambaye kwa hakika neno 'gavana' lilimaanisha Mtei.

Mwalimu Nyerere aliendelea kumwita Mtei Gavana muda wote licha ya kwamba nchi ilipata magavana wengi tu baada yake – Charles Nyirabu, Gilman Rutihinda, Idris Rashid, Daudi Balali, Prof. Benno Ndulu na wengine.

Inaendelea Uk. 21

# Hamba kahle Gavana...

Inatoka Uk. 20

Sina hakika kama kuna hata ukumbi katika majengo ya benki kuu zetu wenye ukumbi wa jina la Mtei.

Kama jibu ni hapana, Benki Kuu itafakari hili. Benki Kuu ina matawi mbalimbali nchini hivi sasa. Nadhani itakuwa jambo jema na murua kwamba moja ya jengo la matawi ya Benki Kuu nchini lipewe jina la Edwin Mtei.

Ikumbukwe tu kwamba ukomavu wa siasa, kutokuwa na woga wa kusimamia unachaomini, ndiyo tafsiri sahihi ya maisha ya Gavana Mtei.

Yeye na wazee – viongozi, wengine waliotutangulia, waliweza kutofautiana bila kuchukiana; waliweza kuwa na misimamo tofauti bila kugombana; waliweza kuwa na mawazo tofauti bila kutekana; na waliweza kuamua tofauti bila kuuana.

Heshima ya mtu, kutotweza utu wa mtu ilikuwa tunu kubwa kwao. Ni wajibu wetu kutafakari na kupita njia yetu ya kutofautiana bila kuvunjiana heshima, bila kupigana, bila kuuana, bila kutekana.

Hiyo ndio njia bora zaidi ya kuwaenzi wazee wetu na leo tunaienzi kwa kumbukumbu zaidi kwa Gavana Edwin Mtei.

***Mwandishi ni Kiongozi (mstaafu) wa Chama cha ACT Wazalendo. 'Hamba kahle- ni maneno ya Kizulu yakimaanisha 'Nenda Salama.'Tanzia hii imehaririwa kidogo kuendana na sera na maudhui ya Chumba cha Habari cha Pambazuko.***

# Chadema yalia...

Inatoka Uk. 9

Mwaka jana 2025, Chadema walianzisha kampeni ya kuchangisha fedha kwa njia ya simu waliyoipa jina la tone tone na kampeni hiyo ilionekana kuwa na mafanikio kwa kuwa wafuasi wao walikuwa wakichangia fedha ili kujenga chama chao.

Wafuasi wa Chadema waliwahi pia kuchangishana zaidi ya shilingi milioni mia moja kwa ajili ya kumnunulia gari la kutembelea, Mwenyekiti wa Chadema, Tundu Lissu ambapo fedha hizo zilikuwa zikichangwa kupitia namba ya Lissu mwenyewe.

Wafuasi wao pia waliwahi kuchangishana fedha kwa ajili ya kuwalipa mawakili waliokuwa wakimtetea aliyekuwa Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, wakati alipokuwa akikabiliwa na kesi ya ugaidi.

Katika miaka ya hivi karibuni, wafuasi wa chama hicho walichanga fedha kwa ajili ya kukijenga chama chao kupitia kampeni maalum iliyopewa jina la Join the Chain.

Mwishoni mwa mwaka jana, wafuasi wa Chadema walimchangia Lissu zaidi ya shilingi milioni 26 kwa ajili ya kumtakia heri ya krismas na kuadhimisha mwaka mpya wa 2026.



Naibu Katibu Mkuu Chadema Bara, Amani Golugwa

Fedha hizo zilikusanywa kwa siku tatu, kupitia simu ya mkononi ya kaka yake Lissu, Alute Mughwai Lissu.

Wakati huohuo, Machi, mwaka 2020, Mahakama Hakimu Mkazi Kisutu, ilimtia hatiani aliyekuwa Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe na wenzake wanane, waliokuwa wakikabiliwa na mashitaka ya kuitisha maandamano ya kusababisha vurugu zilizokuwa chanzo cha kifo cha aliyekuwa Mwanafunzi wa Chuo cha Usafirishaji cha Taifa (NIT), Akwilina Akwilinus.

Baada ya Mbowe na wenzake kutiwa hatiani, waliamriwa kulipa faini ya shilingi milioni 350, ambazo zilichangwa na wafuasi wa Chadema kupitia simu za mkononi ambapo Mbowe na wenzake waliachiwa huru.

■ Habari

# Tanzania kuumia Marekani ikijiondoa WHO

**Na Mwandishi WETU**

TANZANIA ni miongoni mwa nchi za Afrika zitakazoathiriwa na hatua ya Marekani kujiondoa kufadhili Shirika la Afya Duniani (WHO).

Hatua ya Marekani kujiondoa kwenye ufadhili na michango ya fedha kwenye WHO itaumiza pia nchi zingine, hasa masikini, nyingi zikiwa za Afrika.

Marekani, ambaye ni mfadhili mkubwa wa WHO imejiondoa rasmi Januari 22,2026 kwenye ushirika na shirika hilo, hatua ambayo imeibua wasiwasi mkubwa miongoni mwa wataalamu wa afya na jumuia ya kimataifa.

Wengi wana wasiwasi na uimara wa uchumi wa WHO kwa kuwa inategemea zaidi michango na ufadhili kutoka taasisi na nchi tajiri, ikiwamo Marekani.

Ili kukabiliana na hali hiyo ya ukata ulioanza "kung'ata," WHO tayari imepunguza idara zake kutoka 76 hadi 34, huku asilimia 25 ya matumizi yake, yakiondolewa ili kuifanya "iendelee kuwepo" kwa kiasi kidogo cha fedha.

WHO imekuwa ikitoa misaada ya fedha, ushauri na utaalamu kwa nchi nyingi za Afrika, hasa masikini, hatua ambayo sasa inaelezwa kupungua zaidi na pengine "kukoma" kwa baadhi ya maeneo.

Rais wa Marekani, Donald Trump ametekeleza uamuzi huo licha ya kutolewa tahadhari kwamba kujiondoa kwa taifa hilo lenye utajiri mkubwa wa uchumi duniani, kutadhoofisha uwezo wa WHO kukabiliana na majanga ya kiafya pamoja na kuathiri juhudi za kimataifa za kudhibiti milipuko ya magonjwa.

Uamuzi huo pia unatajwa kukiuka sheria za ndani za Marekani ambazo zinaitaka serikali hiyo kulipa deni la takribani dola milioni 260 kwa WHO kabla ya kujiondoa rasmi.



*Katibu Mkuu wa WHO Tedros Adhanom Ghebreyesus*

Kwa mujibu wa sheria hiyo, Marekani inapaswa kutoa notisi ya mwaka mmoja na kuhakikisha imekamilisha malipo yote inayodaiwa na WHO.

Rais Trump alitangaza nia ya kujiondoa WHO siku ya kwanza ya urais wake mwaka 2025 kupitia amri ya kiutendaji, akilalamikia kile alichokitaja kuwa udhaifu wa shirika hilo katika kushughulikia majanga ya kiafya.

Hii ni mara ya pili kwa Rais Trump kuamuru Marekani kujiondoa kuwa mwanachama wa WHO.

Trump alikosoa jinsi shirika hilo la kimataifa lilivyoshughulikia janga la Covid-19 na kuanza mchakato wa kujiondoa kutoka kwa taasisi hiyo yenye makao yake makuu Geneva, Uswisi.

Lakini, Rais Joe Biden alipoingia madarakani, baada ya Trump, kwenye urais wake kwa mara ya kwanza, alibatilisha uamuzi huo.

Agizo hilo la kujiondoa awali, lilieleza kuwa Marekani inajiondoa kutokana na WHO kutoshughulikia janga la Covid-19, ambalo liliibuka Wuhan, China.

Agizo hilo la Rais Trump pia lilisitiza kuwa hatua hiyo ilitokana na malipo yasiyokuwa na uhalali kwa Marekani yanayolipwa kwa WHO ambayo ni sehemu ya Umoja wa Mataifa.

Inaendelea Uk. 23

# Tanzania kuumia...

Inaendelea Uk. 22

**Ufadhili kwa WHO**

WHO iliyoanzishwa mwaka 1948 ikiwa sehemu ya mfumo wa mashirika ya Umoja wa Mataifa, ililenga kuendeleza na kuhimiza afya bora, kuhakikisha dunia inakuwa salama na kuhudumia wale walio katika hatari zaidi.

Shirika hilo limekuwa likipata ufadhili wa lazima na ule wa kujitolea; kwamba kuna fedha ambazo lazima zitolewe na nchi washirika 194.

Kila nchi inatakiwa kulipa kiwango fulani cha fedha kulingana na uimara wake wa uchumi wake na idadi ya watu.

Fedha hizo za michango ya lazima, husaidia kuendesha shughuli za WHO, ikiwamo mishahara na mfumo mzima wa utawala wa shirika hilo kusimamia huduma za afya duniani.

Marekani ilichangia dola za Marekani bilioni 1.284 katika kipindi cha 2022-2023 kuwezesha WHO kuendelea na shughuli zake bila mikwamo.

WHO ilipokea dola za Marekani milioni 363 ikiwa ni ufadhili kipindi cha 2022-2023 kulingana na taarifa katika wavuti ya shirika hilo.

Nchi nyingine kubwa zenye kuchangia zaidi WHO ni pamoja na Ujerumani, Umoja wa Ulaya, Norway, Jamhuri ya Korea, India na Hispania.

Pia yapo mashirika makubwa na yenye ukwasi mkubwa yanayofadhili WHO ikiwamo Bill and Melinda Gates Foundation, ambayo hutoa ufadhili mkubwa kupitia hazina ya The Global Fund.

Mchangiaji mkubwa mwingine ni GAVI, shirika ambalo linajumuisha mashirika ya umma na serikali ambayo yanapigania ushawishi wa kuongeza upatikanaji wa chanjo kwa nchi 73 katika maeneo ya kaskazini kote duniani.

**Ufadhili mkubwa kutoka WHO**

Sehemu kubwa ya fedha za WHO, pamoja na kutumika kwenye utawala na huduma za kimataifa, yapo maeneo ambayo hufaidi zaidi misaada yake, yakiwamo yale ya eneo la Mediterranean, kwa nchi 22 kutoka Morocco hadi Pakistan.

Eneo hilo limepokea karibia dola milioni 201 za Marekani, sawa na asilimia 36 ya fedha zilizotolewa na Washington kwa miaka ya hivi karibuni.

Eneo jingine ni Afrika, ambayo inajumuisha nchi 47 kwa bara hilo huku ufadhili kutoka Marekani ukiwa ni jumla ya dola milioni 151 za Marekani.

Eneo la jingine linalopokea ufadhili wa Marekani ni makao makuu ya WHO, ambayo yanapokea karibia dola milioni 101 za Marekani, kiasi hicho kikitumiwa kwa uendeshaji wa shughuli zake na kampeni kadhaa za masuala ya afya.

Ni asilimia kidogo tu ya ufadhili wa Marekani karibia dola 280,000 sawa na takriban asilimia 0.5, ambazo zimetumika kufadhili shughuli za WHO kwa nchi za Amerika ya Kusini na zile za Caribbean.

Upande wa kampeni za afya, zaidi ya robo ya ufadhili wa Marekani zimetengwa kukabiliana na polio duniani (dola milioni 158 sawa na asilimia 27 ya fedha ilizotoa kwa ujumla).

Dola milioni 100 zimetumika katika miradi ya kuwezesha watu kupata afya bora na ulaji sahihi, huku dola milioni 44 za Marekani zikitumika katika miradi ya utoaji wa chanjo dhidi ya magonjwa yanayoweza kuzuilika.

Na dola milioni 33 zinazohitajika kukabiliana na kifua kikuu zikiwa zimeendelea kutumika.

Lakini hiyo ni baadhi tu ya miradi kwa sababu pia kuna fedha zilizotengwa kukabiliana na Ukimwi na hepatitis hadi uzuiaji na udhibiti wa kutokea kwa majanga pamoja na fedha za kukabiliana na magonjwa ya kitropiki hadi afya ya uzazi, upatikanaji wa dawa na miradi mingine mingi.



*Makao Makuu ya WHO*

Kilinge cha Mawasiliano



Na Loth MAKUZA

# Uhusiano na Umma ni imani, huanza na uhalisia

UHUSIANO na Umma (PR), siyo taarifa kwa vyombo vya habari. Wala siyo kaulimbiu. Na pia siyo zimamoto baada ya nyumba tayari kuanza kuungua.

Uhusiano na Umma (PR) ni simulizi. Ni uhusiano thabiti baina ya pande mbili. Zaidi ya yote, ni imani.

Lakini imani haijengwi kwa maneno matupu. Uhusiano na Umma (PR), unapofanya jambo lolote husikika zaidi kuliko maneno matupu.

Huu ndio ukweli mchungu, kwamba ukifanya vibaya na ukasema vibaya - Uhusiano na Umma (PR) mbaya; ukifanya vibaya, lakini ukasema vizuri - bado Uhusiano na Umma (PR) mbaya.

Ukifanya vizuri, lakini ukasema vibaya, Uhusiano na Umma (PR) mbaya pia na unapofanya vizuri na kusema vizuri, ndipo unajenga Uhusiano na Umma (PR) vizuri.

Ndiyo maana mengi yanayojulikana kama "migogoro na majanga katika mashirika" siyo matatizo ya ki-PR hata kidogo. Ni matatizo ya taasisi zenyewe.

PR haiwezi kurekebisha bidhaa isiyokuwa na ubora stahiki. Haiwezi kufunika tabia zisizo za kimaadili. Haiwezi kusafisha uhalifu.

Hakuna ujumbe mzuri unaoweza kuokoa mfumo uliooza. PR hufafanua uhalisia, haiubadili uhalisia kuwa kitu tofauti.

Sasa, PR sahihi inaonekana vipi kwa kampuni zinazotaka kuishi katika mazingira ya kibiashara ya Tanzania?

Inaanzia kwenye utafiti. PR bila utafiti ni kubahatisha. Ni lazima ujue ni waandishi gani wana umuhimu, wanaandika nini, wanafanyaje kazi, na wanatafuta chanzo gani ya habari.

Ieleweke kuwa kuheshimu taaluma ya uandishi wa habari, ni chanzo kikuu cha kusikilizwa. Na ukipuuza habari yako itakufa kimyakimya.

Baada ya hapo kuna upimaji. Usichopima, kitu hutajua ubovu wake, hivyo huwezi kukirekebisha.

**Ukisikiliza mapema, unaweza kuzima cheche kabla haijawa moto. Pia unatambua mwelekeo kabla ya wapinzani wako.**

PR siyo hisia, bali ni matokeo. Malengo (KPIs) hubadilisha kelele kuwa mkakati. Malengo yaliwekwa mahsusi kwa PR, kwa sababu sifa, uaminifu na mwonekano vinahitaji nidhamu.

Matumaini si kipimo na ieleweke kuwa PR kamwe haina mwisho. Ni mchakato wa muda mrefu wa uthabiti, kutatua changamoto halisi za wadau na kuwasiliana kwa uwazi, mara kwa mara, na kwa uaminifu.

Tukifahamu haya, mtazamo hubadilika. Hapo ndipo uaminifu huzaliwa. Hapo ndipo chapa hupata watetezi, siyo watazamaji wa muda mfupi.

PR haiwezi kufanya kazi peke yake. Katika mazingira ya kidijitali yaliyochanganyika, mawasiliano lazima yawe karibu na uongozi, wafanyakazi, timu za masoko na washirika.

PR siyo kuzungumza tu, bali ni kusikiliza. Ufuatiliaji wa vyombo vya habari, hisia za umma na sehemu ya sauti zao hufichua jinsi chapa yako inavyoonekana kweli, siyo jinsi unavyotamani ionekane.

Ukisikiliza mapema, unaweza kuzima cheche kabla haijawa moto. Pia unatambua mwelekeo kabla ya wapinzani wako.

PR bora ni ile inayotangulia, siyo ile inayokimbiza matukio.

Kusubiri habari ni mkakati wa kushindwa. Wataalamu wa kweli hujenga simulizi kabla ya dharura kuwalazimisha kujitetea.

PR huishi na kufa kwa imani hasa kwa waandishi wa habari. Majukwaa ya kidijitali ni muhimu, lakini hayawezi kuchukua nafasi ya uhusiano wa kibinadamu.

Kila mtu anaweza kupaza sauti. Wachache wanaweza kusikilizwa. Uhusiano mzuri hubadilisha kelele kuwa habari.

***Mwandishi wa safu hii ni mtaalamu wa uhusiano na Umma (PR). Anapatikana kwa namba: 0625 704 995 na kupitia email; projects@lothmakuza.co.tz***



*Mafundi wakiendelea na ujenzi wa ukuta katika eneo wazi lisiloruhusiwa la Ukanda wa Kijani katika Mtaa wa Kibaga, Kata ya Kinyerezi, Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam juzi. (Na Mpigapicha Wetu).*

# Aliyevamia eneo la wazi, bado 'akomalia' ujenzi

**Na Mwandishi WETU**

MFANYABIASHARA aliyevamia eneo la ukanda wa kijani lililotengwa kisheria katika Mtaa wa Kibaga, Kata ya Kinyerezi, Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam, ameendelea na ujenzi licha kukosa kibali cha kufanya hivyo.

Mtu huyo ameonyesha kinachoelezwa na mamlaka kuwa kiburi kwa kuendelea na ujenzi licha ya mamlaka husika kumtaka asitishe ujenzi huo.

Wiki iliyopita, gazeti hili liliandika kuhusu uvamizi huo na kubainisha kuwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, kupitia Idara ya Mipango Miji iliweka notisi inayoweka wazi kuwa ujenzi unaoendelea katika eneo hilo hauna kibali, hivyo ni batili.

Notisi ya zuio la ujenzi ilitolewa Novemba 19, 2025 ikiwa na Kumb No DCC/HD.101/31 ikitoka kwa Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam kwenda kwa Gervas Shayo ikimpa amri ya kubomoa na kuondosha ujenzi uliofanyika kinyume cha sheria.

Notisi hiyo ilisainiwa na Mhandisi Lusekelo A. Mwakyami kwa niaba ya mkurugenzi, ilisema kwa kuwa amejenga ukanda wa kijani ambalo ni kosa chini ya kanuni ya 139 (1) ya serikali za mitaa, mamlaka za miji, (udhibiti wa ujenzi) ya mwaka 2008, hivyo aliamriwa ndani ya siku 14 tangu kupokea amri hii awe amebomoa na kuondosha ujenzi huo.

Hata hivyo ikiwa imekaribia mwezi wa tatu sasa, notisi hiyo haijatekelezwa na muhusika anaendelea na ujenzi, na kuzua sintofahamu ya nini kinaendelea katika mamlaka za halmashauri ya jiji la Dar es Salaam ambao ndiyo wenye dhamana za kusimamia na kuhakikisha sheria zinalindwa na kutekelezwa.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Pambazuko lilifika tena katika eneo hilo na kushuhudia mafundi wakiendelea na ujenzi wa ukuta kuzunguka nyumba ambayo ujenzi wake kwa nje unaonekana kuwa umekamilika.

Ukuta huo unajengwa wastani wa mita moja kutokea kwenye mfereji wa maji machafu yanayopita chini ya karavati kubwa linalotenganisha barabara ya lami ya Kinyerezi - Ulongoni hadi Gongolamboto.

Inaendelea Uk. 26

Habari

# Aliyevamia eneo la wazi...

Inatoka Uk. 25

Sambamba na hilo, Pambazuko pia limeona kuwapo maandalizi ya miundombinu ya kuvuta maji kuelekea kwenye eneo hilo la ujenzi.

Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Elihuruma Mabelya, hakupatikana kuzungumzia suala hilo kwani simu yake iliita bila kupokewa, na hata alipotumiwa ujumbe mfupi wa maandishi hakujibu.

Haya ni kati ya maswali ambayo Gazeti la Pambazuko lilitaka kupata majibu kutoka kwa mkurugenzi wa jiji hilo;

1. Nini maoni yako kuhusu mtu aliyevamia na kujenga nyumba eneo lisiloruhusiwa kisheria (green belt), Mtaa wa Kibaga Kata ya Kinyerezi.

2. Novemba 19, 2025, ofisi yako ilitoa notisi kwa mhusika na kumpa siku 14 kubomoa mwenyewe, vinginevyo atafikishwa mahakamani, je, kitu gani kimezuia utekelezaji wake na sasa ni miezi mitatu imepita?

3. Kuna sheria/kanuni yoyote imebadilishwa na Halmashauri yako kuruhusu maeneo ya wazi na ukanda wa kijani kuvamiwa na kubadilishwa matumizi yake?

Awali, mmoja wa maofisa Mipango Miji Kanda ya Kinyerezi katika halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ambaye jina lake tunalo aliliambia Pambazuko kuwa ofisi yake haijatoa kibali chochote kuruhusu ujenzi huo, na kinachoendelea kwenye eneo hilo ni ukiukwaji wa sheria.

Pambazuko limebaini kuwapo msigano kwa baadhi ya watendaji wa jiji hilo kuhusu jambo hilo, huku wengine wakionyesha kutoridhishwa na namna linavyoshughulikiwa na 'wakubwa wao.'

Mmoja wa maofisa wa Idara ya Mazingira ya Jiji la Dar es Salaam ambaye hakutaka jina lake litajwe gazeti alisema kupitia Ofisi ya Mipango Miji Kanda namba nne ya Kinyerezi wamejiridhisha wazi kwamba hakuna kibali kilichotolewa kwa ajili ya ujenzi kwenye eneo hilo.

"Huyo mtu anayejenga kwenye eneo hilo hana kibali, na anadai kuwa alitoa fedha shilingi 200,000 kwa ajili ya kibali na kupewa risiti, lakini sio kweli, fedha hiyo ilikuwa kwa ajili ya uchunguzi, na alitumia hiyo risiti na kumpelekea Mkurugenzi wa Jiji, nadhani mkurugenzi alijua hicho ndicho kibali, ndiyo maana anashindwa kuchukua hatua.

"Ni vyema sasa mkurugenzi atushirikishe sisi maafisa wake ili tuweze kumpa ukweli wa jambo hilo, tunajua hilo jambo lilipitia ngazi zote, hatua zote za kisheria zilifanyika juu yake ikiwamo demolition order (agizo la ubomoaji) hivyo tunajiuliza hiki kiburi kinatoa wapi"alihoji Ofisa huyo.

"Hilo eneo ni sehemu ya kupanda maua, miti na kuifanya iwe ya kijani, siyo vinginevyo"alisisitiza mtaalam huyo wa mazingira.

Wiki moja baada ya Pambazuko kuripoti suala hili, Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Faraja Nakua, aliiandikia Kampuni ya Group five Eathworks (T) LTD ya Dar es Salaam ilipewa kibali cha kutunza eneo hilo tangu Julai 2013.

Barua yenye kumb No. DCC/EU.1/2 ya Januari 19, 2026 ilitoa maelezo mawili kwa kampuni hiyo ikitakiwa kutoa maelezo ya maandishi kwa nini kibali alichopewa kisifutwe, lakini pia kwa nini asichukuliwe hatua za kisheria kwa kutofuata masharti ya kibali na kusababisha uharibifu wa eneo unaotokana na shughuli tofauti na malengo ya utunzaji wa eneo hilo.

Akizungumza na Pambazuko mmoja wa viongozi wa Group Five Eathworks (T) LTD, Jonathan Kaihula, alisema ameshangazwa na barua hiyo ya Kaimu Mkurugenzi wa jiji la Dar es Salaam kwa sababu imekwepa wajibu wake.

Alisema eneo hilo alikabidhiwa na kulitunza kwa mujibu wa kibali husika kwa kupanda miti ya matunda kwenye husika na kulifanya liwe la kijani muda wote, lakini katika hali ya kushangaza mvamizi alipoanza ujenzi alifyeka mazao yote na picha zote anazo.

"Msuguano uliopo ni wa kwa nini wameruhusu ujenzi kuendelea katika eneo lisiloruhusiwa kisheria. Hii ya kutishia kufuta kibali cha utunzaji wa mazingira hakihalalishi sheria za mipango miji kuvunjwa. Niwaombe watimize wajibu wao kwa mujibu wa sheria," alisema Kaihula.



Na Rashid MTAGALUKA

# Barabara msingi uliopuuzwa maendeleo ya Mchinga

ASUBUHI inayoanza kwa mvua, siyo tukio geni kwa wananchi wa Mchinga. Ardhi huloa, mito hujaa, na barabara hubadilika kuwa vijito vya tope.

Katika kijiji cha Namkongo, baba mmoja alisimama pembeni ya njia iliyokatika akimtazama mwanawe akichelewa shule.

Sare ilikuwa safi, madaftari mapya, lakini safari haikuwezekana. Shule ipo, majengo yapo, lakini njia ya kuyafikia haipo. Hapo ndipo simulizi la maendeleo ya Mchinga linapopata mshikamano wa maswali kuliko majibu.

Hakuna ubishi kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imefanya kazi kubwa katika sekta ya elimu na afya. Mabweni, madarasa, shule mpya za amali, zahanati na vituo vya afya ni ushahidi wa dhamira ya utekelezaji wa Ilani ya CCM.

Jimbo la Mchinga limebahatika kuguswa moja kwa moja na juhudi hizi, na viongozi wake wakiwemo mbunge na viongozi wa serikali za mitaa wanastahili pongezi.

Lakini maendeleo haya yanapokosa kiungo muhimu cha kuyaunganisha na mwananchi, thamani yake hubaki kwenye karatasi na picha za ziara.

Kwa wananchi wa Nangaru, Matapwa, Lihimilo, Dimba, Mvuleni, Kiwawa na maeneo mengine, changamoto siyo uwepo wa shule au vituo vyha afya, bali ni jinsi ya kufika huko. Kila mwaka, mvua zinaponyesha, huduma hukatika.

Wagonjwa hushindwa kuwahi matibabu, wajawazito hubebwa juu ya pikipiki au machela, mazao hushindwa kufikishwa sokoni, na uchumi wa kaya huporomoka. Barabara mbovu hugeuka kuwa adui wa maendeleo yote mengine.

Ukweli huu unatupeleka kwenye hoja ya msingi kwamba, vipaumbele vya maendeleo lazima vitokane na uhalisia wa wananchi.

Elimu na afya ni nguzo kuu za maendeleo ya binadamu, lakini miundombinu ya barabara ndiyo mishipa inayosafirisha uhai wa huduma hizo. Bila barabara, shule hubaki majengo, zahanati hubaki kuta, na vituo vya afya hubaki alama kwenye ramani.



*Mwananchi akijaribu kuvuka kwenye Daraja la Nangaru lililojaa maji yaliyofunika barabara hiyo na kuzuia namna ya kupitika kwa urahisi.*

Mfano wa mtu mwenye njaa kali unatoa picha iliyo wazi. Unapomletea suti ya gharama kubwa badala ya chakula, hujafanya kosa, lakini hujagusa tatizo lake la msingi.

Vivyo hivyo, kuwekeza fedha nyingi kwenye majengo bila kutatua changamoto ya barabara ni kuchelewesha suluhisho la shida halisi ya wananchi. Wananchi hawapingi maendeleo, bali wanahoji mwelekeo wa vipaumbele.

Safu hii haukusudii kubeza jitihada za serikali wala kuhoji dhamira ya viongozi. Ni mwito wa kutazama maendeleo kwa macho ya mwananchi wa kawaida.

Barabara zikiboreshwa, shule zitafanya kazi kwa ufanisi, vituo vya afya vitaokoa maisha, na uchumi wa vijiji utaimarika. Ndipo utekelezaji wa Ilani utakapopata maana yake halisi.

Maendeleo ya Mchinga hayahitaji kuanza upya, bali yanahitaji kuunganishwa. Barabara ni daraja kati ya sera na maisha ya wananchi. Bila daraja hilo, maendeleo hubaki kuwa hadithi nzuri, isiyofikika kwa yule anayeyahitaji zaidi.

***Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com***

Habari

# Tanesco yaahidi kumsaka aliyedai kuweka umeme kwa wanavijiji



Mkurugenzi Mtendaji wa Tanesco, Lazaro Twange

Na Mwandishi WETU

WANANCHI wa Kijiji cha Kashenge, Kata ya Mafumbo, Tarafa ya Kamachumu, wilayani Muleba, Kagera wamedai kutapeliwa na mtu aliyejifanya ni mtumishi wa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) aliyewaahidi kuwapatia umeme kupitia miradi inayotekelezwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

Mtu huyo aliwashawishi wanavijiji hao kuchanga fedha ambazo walimpatia kwa ahadi kuwa atawasaidia kuunganishiwa umeme.

Lakini ni mwaka mmoja na nusu sasa, watu hao hawajaunganishiwa umeme na kilio chao kimeshindwa kusikika na kufanyiwa kazi.

Wananchi hao wamelieleza Pambazuko kuwa, Juni 2024, waliingia makubaliano na Aniceti Muganyizi ambaye alijitambulisha kwao kuwa ni mmoja wa wakaguzi wa Tanesco ngazi ya mkoa, ambapo aliwakusanya na kuwashawishi wampatie fedha shilingi 1,660,000 ili awasadie kupata umeme katika eneo la Kalindwa ambalo halikupata umeme kwenye mradi wa awali kijijini hapo.

Wananchi hao wamesema kwa kuwa mtu huyo ni mzaliwa wa kijiji jirani cha Mafumbo ndani ya kata hiyo, walimwamini na kumpatia fedha hizo kwa awamu tofauti.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, mmoja wa wananchi hao, Eliud Emmanuel, alisema katika makubaliano hayo, awamu ya kwanza walichangishana na kumpatia shilingi 240,000, na mwezi uliofuata, yaani Julai 2024, walimpatia shilingi 450,000.

Siku hiyo aliahidi pia angewaletea nguzo sita ikiwa ni maandalizi ya kuletewa umeme kwenye eneo lao lililopo katikati ya kijiji hicho, lakini hakuzileta nguzo hizo.

Aidha, katika mgao huo wa fedha, Muganyizi aliwaambia wananchi hao kuwa, Shilingi 203,000 wanapaswa kumpatia mtunza stoo ili aruhusu vifaa kutoka. Fedha hizo alitumiwa kwenye simu yake ya mkononi, na baadaye walimtumia tena shilingi 103,000 kwa njia ya simu.

"Tukiwa maeneo ya Itongo (Amuchwezi), karibu na Mji wa Kamachumu tulikutana na Muganyizi baada ya kupigiana simu ambapo nilimkabidhi fedha Shilingi 500,000 na siku hiyo nikiwa na pikipiki yangu alikwenda kunionyesha nguzo eneo la Kyamalebe ambao ni wastani wa kilometa nne kutoka mji wa Kamachumu.

"Katika eneo hilo kulikuwepo na nguzo nyingi pembezoni mwa barabara, alinionyesha akasema sisi tutapata nguzo sita na kama tungepitia utaratibu wa kawaida kila nguzo tungeweza kuuziwa kwa shilingi 321,000, lakini kwakuwa anatusaidia basi tutaingizwa kwenye mradi wa REA ambao gharama yote haifiki shilingi milioni mbili.

"Awali Muganyizi aliniambia anawasiliana kwa simu na dereva mwenye gari la kubeba hizo nguzo lakini baadaye akasema mwenye gari amepata dharura, hivyo nguzo tutazichukua siku nyingine," alisema.

Oktoba mwaka jana, Pambazuko lilimtafuta Muganyizi ili atolee ufafanuzi tuhuma hizo. Bila kumung'unya maneno, alikiri kupokea fedha hizo za wananchi, kwa ahadi ya kuwasaidia kupata umeme kwenye kitongoji chao.

Inaendelea Uk. 29

# Tanesco yaahidi...

Inatoka Uk. 28

Hata hivyo, alimuomba mwandishi wa habari hizi ampe muda ili awasiliane na wenzake kutoka Tanesco ambao alishirikiana nao ili warudishe fedha walizowachangisha wananchi kwa kuwa jambo hilo limeshindwa kufanyika.

"Kwa sasa mimi sipo tena Tanesco zaidi ya miezi tisa sasa, ukweli ni kwamba niliwapatia vijana fedha kwa kuwa mimi nimehama na kwa sasa nipo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa kazi maalum…"

"Ni kweli fedha hizo mimi nilizichukua, niliwapatia wenzangu waliokuwa kwenye mradi wa REA, na muda ulivyokwenda niliwaambia hao wananchi kwamba suala hilo limeshindikana hivyo nafanya juhudi za kuwarudishia fedha zao," alisema Muganyizi.

Aidha, Desemba mwaka jana, Pambazuko lilimuuliza tena Muganyizi amefikia wapi kuhusu kurudisha fedha hizo za wananchi.

"Kwa sasa siko tena Tanesco, nimehamishiwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kagera kwa kazi maalum, hata hivyo hawa wenzangu niliowakabidhi suala la umeme nao wananiambia hawana pesa yoyote kwa sasa, sijui hata tunafanyaje!" alisema.

Uchunguzi wa Pambazuko umebaini kuwapo sauti inayodaiwa ni ya mazungumzo kati ya Muganyizi na wananchi wakijadiliana kuhusu suala hilo huku yeye akisema mpango huo wa kuwasaidia kupata nishati ya umeme sasa umeshindikana.

Januari 22, 2025, Pambazuko lilizungumza na Meneja wa Tanesco Mkoa wa Kagera, Tawakal Twahila, kuhusu suala hilo ambapo alisema wakati huo alikuwa safarini nje ya kituo chake cha kazi, lakini amelipokea, atalifanyia kazi na kulitolea ufafanuzi baadaye.

Alisema endapo kuna watumishi ndani ya shirika hilo wanaojihusisha na utapeli kwa wananchi, basi hatua stahiki zitachukuliwa dhidi yao.

"Nakushukuru nimepata taarifa hiyo, kwa sasa nipo nje ya ofisi, nikirudi ofisini Jumatatu (leo), nitalifanyia kazi kupitia maafisa wetu wa kitengo cha usalama, tutafanyia uchunguzi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya usalama tukiwabaini watachukuliwa hatua stahiki…"

"Watu wa aina hiyo huenda ni matapeli au wamewahi kufanya kazi Tanesco, hawa tutashughulika nao. Lakini pia tutafuatilia kwenye hicho kijiji kinachohitaji umeme ili tuone, kinafikiwaje ili waweze kupata haki yao," alisema meneja huyo wa Tanesco mkoa wa Kagera.



*Waziri wa Fedha Balozi Khamis Mussa Omar, akiweka shahada la maua kwenye kaburi la Edwin Mtei.*

■ Utalii

# Maajabu usiyoyajua kuhusu faru John, Fausta



Faru Fausta



Faru John

Na Mwandishi WETU,

KATIKA ulimwengu wa Wanyama, kuna historia na maajabu ya aina yake.

Na maajabu hayo yanagundulika baada ya tafiti mbalimbali za kitaalam kuhusu wanyama hao.

Leo katika makala haya tutaangalia maajabu ya mnyama faru ambaye anapatikana kwenye mbunga za taifa hususan ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro.

Katika eneo hilo kuna historia isiyofutika ya faru wakubwa wawili ambao waliishi katika hifadhi hiyo kwa mda mrefu zaidi.

Faru hao ni Fausta aliyezaliwa mwaka 1965 na kufa mwaka 2019 na faru John aliyezaliwa mwaka 1978 na kufa mwaka 2016.

Ngorongoro imewaweka kwenye historia faru hao ili kuwaonesha watanzania umuhimu wa kuhifadhi faru ambapo idadi yake ndani ya hifadhi hiyo inazidi kuongezeka na kuvutia watalii kutoka ndani na nje ya nchi na hivyo kuwa na mchango mkubwa katika uingizaji wa fedha za kigeni.

Faru John ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro alijulikana pia kama bingwa wa mapenzi ama 'dume la mbegu' kutokana na kuweza kuizunguka hifadhi yote akitafuta faru majike ili aweze kujamiiana nao huku upendo wake ukitawaliwa na wivu wa kupindukia.

Tabia nyingine ya faru huyo ilikuwa ni utawala wa muda mrefu ndani ya hifadhi hivyo alikuwa chanzo kikubwa cha migogoro na kutaka kila faru jike awe naye peke yake hali ambayo mwaka 2011 alimuua faru Fausta kwa kugombea jike, hii inadhihirisha ule usemi wa Kiswahili usemao 'mapenzi yanaua'.

Tofauti na faru John, faru Fausta ndiye faru pekee aliyeweza kuishi ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa muda mrefu wa miaka 54 na inasemekana pia amevunja rekodi ya kidunia kuwa miongoni mwa faru wachache weusi walioishi miaka mingi.

Licha ya kupendwa na madume, faru Fausta, hakubahatika kupata mtoto na kwa mujibu wa wataalam wa wanyama haikubainika ni kwa nini faru Fausta katika umri wake wote wa miaka 54 hakujaaliwa uzazi.

Kisayansi faru anaweza asipate mtoto kutokana na kuwa na matatizo katika mfumo wa uzazi ikiwa ni pamoja na kuchelewa kupata mimba ambapo faru akiwa na hali hiyo katika umri unaotakiwa anakuwa na homoni kiasi kidogo za jike na hivyo kushindwa kupata mimba.

Lakini kitendi hicho cha kutoshika mimba kinaweza pia kuwa sababu ya faru huyo kuishi maisha marefu.

Wataalam wanasema kuwa faru Fausta inawezekana aliishi muda mrefu kwa sababu hakuwa na msongo wa mawazo wakati wa kushika mimba, kulea watoto wala kunyonyesha zaidi ya 'kula bata' na kushiriki mapenzi na faru wenzake.



**Tunakaribisha barua. Tuma kupitia**

**Tuandikie kero ya eneo lako kupitia WhatsApp namba; +255 712 792216 au tutumie kupitia email; info@pambazuko.or.tz**

## Barabara Mailimoja – Baobab, nini tatizo?

**Mhariri,**
HII ni mara ya tatu naleta tena kero kuhusu barabara inayotoka Mailimoja hadi Baobab kuelekea Bagamoyo kupitia Kata ya Pangani, Halmashauri ya Kibaha Mji. Barabara hii ni mbovu kupindukia.

Ahadi zimekuwa nyingi kutoka kwa viongozi kuwa itajengwa kwa kiwango cha lami, lakini tangu mwaka juzi hakuna kinachoendelea.

Tunaomba kwa mara nyingine mamlaka itutatulie kero hii.

**Anna Rweyemamu,**
**Kibaha,**
**0783682018**

## Mgao wa umeme upo Goba?

**Mhariri,**
KATIKA miezi ya karibuni umeme umekuwa ukikatika mara kwa mara katika maeneo ya Goba, Dar es Salaam.

Kwa mfano, umeme ukiwepo asubuhi, lazima jioni tutalala bila kuwa na nishati hiyo - giza.

Hii hali inatuletea kero na usumbufu mkubwa kwa sababu vifaa vyetu vya umeme pamoja na vyakula vinaharibika kwenye friji.

Ni vyema Taneso wangetuambia kwamba kuna mgao ili tujipange, kuliko Kwenda bila taarifa.

**Eveline Joseph**
**Goba, Dar es Salaam.**

## Barabara Shule Maalum ya Wasichana Dar es Salaam – ‘ya Samia’ itengenezwe

**Mhariri,**
KWANZA napenda kupongeza umahiri wa gazeti lako la Pambazuko kwa kuandika habari nzuri, za uhakika na zenye kubeba uhalisia wa mizania ya matakwa ya uandishi.

Tangu nianze kusoma gazeti lako, sijajuta.

Napenda kupitia Pambazuko kufikisha kilio changu na wengine wengi tunaotumia barabara ya Njeteni, iliyoko eneo la Kwembe, Ubungo Dar es Salaam.

Barabara hiyo inayoelekea Shule Maalum ya Wasichana ya Dar es Salaam, almaarufu – Shule ya Samia, ni mbovu mno na inahitaji matengenezo ya haraka kabla mvua hazijaanza kwani ndiyo itashindwa kupitika kabisa.

Miaka nenda-rudi, sisi wakazi wa maeneo hayo, tunaotumia barabara hiyo, ni kama tumetelekezwa na watendaji wanaohusika na barabara, tumepiga sana kelele kuomba itengenezwe kwa kiwango hata cha changarawe, lakini hakuna anayejali.

Tunaomba sasa wakubwa wetu wa Dar es Salaam, na hasa kupitia Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, wizara watusaidie ili na sisi tuone matunda ya kuwa Watanzania.

**Rashid Hamduni Hassan,**
**Eneo la Kwahovyo, Kwembe**

## Habari Kuu

# 'Tukosoane,...

Inatoka Uk. 6

Askofu Makundi alisisitiza kuwa endapo kuna mahali watu wamegombana, ni vyema wakae, wazungumze na wote watubu pale walipokosea.

**Waziri Mkuu Nchemba**

Akizungumza kwa niaba ya serikali, Waziri Mkuu Dkt. Mwigulu Nchemba alisema Mzee Mtei amekuwa mtu pekee kushika nyadhifa zote za juu katika Wizara ya Fedha kwani amekuwa Gavana, Waziri, Katibu Mkuu na kuwakilisha nchi kimataifa huko IMF.

Alisema Mtei alikuwa mcha Mungu, muadilifu, mchapa kazi ambapo kutokana na kutambulika na weledi wake, mwaka 1982 serikali iliidhinisha kutumika kwake katika nafasi kubwa kwenye shirika la kimataifa ambazo nchi wanachama hupewa nafasi ya kuwa na mwakilishi.

"Mtei alikuwa mwanzilishi wa Chadema na amekuwa mwanasiasa ambaye amechangia kwa kiasi kikubwa katika kujenga demokrasia na Rais Samia Suluhu Hassan amenielekeza mimi niliye mtendaji mkuu wa serikali, kuhakikisha kipande cha njia nne kutoka Tengeru, Usa River kwenda Kia ambapo tayari usanifu umeshakamilika, utaratibu uendelee, kama sehemu ya kuenzi kazi, kupenda maendeleo na maono ambayo ilikuwa tabia ya Mtei.

"Kwa kuwa alipenda haki na shamba la Mringa Estate lilikuwepo hapa, nimeambiwa nisimamie kumaliza mgogoro uliosababishwa na wanunuzi ambao walibadilisha mpaka na kuingia kwenye mzozo na wananchi, hivyo naelekeza ndani ya mwezi mmoja wawe wamerekebisha yale maeneo yaliyofutwa wahusika wapewe haki yao," alisema.

**Tutuba: Alikuwa mwadilifu**

Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Emmanuel Tutuba, alimtaja Mzee Mtei kuwa mtu aliyekuwa na familia imara na hofu ya Mungu na ndivyo vilivyomuimarisha.

"Alikuwa mtu aliyemtumainia Mungu katika kila jambo. Aliweka misingi thabiti tangu kuanzishwa kwa benki kuu ambayo ndiyo inayotuwezesha kufaya kazi vizuri, hivyo tunaiomba jamii kuyaenzi yale mema aliyoyafanya wakati wa uhai wake, kwa alama ya kipekee aliyoiacha," alisema.

Tutuba alisema alibahatika kumtembelea Mzee Mtei mara kwa mara na alimsisitiza kuendelea kupendana na kusaidiana katika shida na raha.

**Jenerali Ulimwengu**

Akitoa salamu kwa niaba ya marafiki wa Chadema, mchambuzi mahiri wa siasa, Jenerali Ulimwengu alisema amekuwa na urafiki na Mtei kwa muda mrefu, na katika mambo mengi aliyomfundisha, moja kubwa lilikuwa kutopenda kitu kinaitwa "uswahili" na hilo alilithibitisha kwake alipompa kazi ya kutoa maelezo kuhusu kitabu chake cha From a Goat Head to a Governor (Kutoka kuchunga mbuzi hadi kuwa Gavana). "Na ukweli ni kwamba kwa Mwalimu ile kujiuzulu ilikuwa ni njia yake ya heshima ya kukufukuza kazi, anakwambia usisubiri barua yangu, anakwambia kwamba kaandike barua kwamba umejiuzulu, usilazimishe nikufukuze,"alisema Ulimwengu.


**Heche: Hatutaacha ujasiri**

Pamoja na kuwasilisha salamu za Mwenyekiti wa Chadema, Tundu Lissu ambaye yuko gerezani kutokana na kesi ya uhaini inayomkabili, Makamu Mwenyekiti wa Chadema, John Heche alisema Mtei alikuwa mtu jasiri aliyesimamia kile anachokiamini hadi mwisho bila kujali gharama, hivyo hawataacha ujasiri huo.

Alisema hatua ya kuacha uwaziri wa fedha kwa sababu alitofautiana na rais wakati huo ilikuwa ni sehemu ya mfano, japokuwa sasa hivi hakuna anayeweza kufanya hivyo, zaidi ya kujenga fitina anapotaka ili waende mbele.

"Tunaona sasa hivi watu wakitofautiana kwa hoja unapotea na hutaonekana, siyo mzaha lakini sisi tunakutwa na haya kwa sababu tunafuata misimamo yake. Chama chetu hakitayumba hata tone katika kusimamia misimamo ya kujenga nchi na uchumi shirikishi,"alisema Heche.

Mzee Mtei – kwa utaratibu wa umoja wa magavana wastaafu Tanzania, ndiye mlezi wa wastaafu.




Je, wewe unapenda kujifunza na kupata uelewa wa mambo anuani?

Kama jibu ni ndiyo, basi kuwa tayari kupata nakala yako ya vitabu vifuatavyo kutoka kwa mwandishi Simon Martha Mkina;

1. Mwalimu Nyerere Hazina Tanzania

- Kitabu hiki kilichapishwa mara ya kwanza 1999 mara baada ya kufariki kwa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Sasa kinachapishwa kwa kurejerewa na kuwemo kwa mambo kadhaa ambayo hayakuwahi kuwemo kwenye kitabu cha awali.


2. Ink meets Mic meets Camera: A Journalism Primer

- Kitabu hiki kinachapishwa kwa mara ya kwanza ikiwa ni mwongozo wa mafunzo kwa waandishi wa habari wapya na hata wale wanaotaka kujifunza zaidi kuhusu umahiri katika uandishi wa habari wa magazeti, redio, blog, televisheni (ikiwamo zile zinazotangaza mitandaoni).

Nini kifanyike: Ikiwa utapenda kupata nakala ya vitabu hivi - au kimoja wapo, unatakiwa kuandika ujumbe mfupi kwenye simu yako na kutuma kwa namba hii: 0754 020880. Taja kitabu unachopenda kukipata mara baada ya kuanza kuuzwa. Vitabu hivi vitauzwa kwa njia ya upekee kwa wale wanaoandika ujumbe kwanza kabla ya kuanza kuuzwa kwenye maduka ya vitabu Tanzania nzima. Bei ya kitabu kuhusu Mwalimu Nyerere ni Shilingi 20,000 na kile cha mafunzo ya uandishi wa habari ni Shilingi 30, 000.

Karibuni sana tuendelee kujifunza.

Elimu ni bahari!



Na Anti MSHAURI





# Timiza malengo kwa kutenda, hakuna miujiza

HABARI za leo msomaji wa safu ya uhusiano. Karibu uweze kujipatia maarifa mbalimbali kupitia safu hii.

Bila shaka uko na afya njema na umeuanza vizuri mwaka mpya wa 2026. Nakupa pole wewe unayepitia changamoto yoyote, nikiamini kwa uwezo wa Mungu utakaa sawa.

Leo nitazungumza namna ya kuweka mipango yako vyema ili kutimiza malengo yako.

Ni wazi kwamba Januari ni mwezi wenye pilikapilika na majukumu mengi ya kimaisha na ili kufanikisha mipango yako unapaswa kujipanga kikamilifu ili kuondokana na changamoto mbalimbali.

Kwa kawaida mwaka mpya unapowadia kila mtu anakuwa na shauku ya kujiwekea maazimio na malengo kadhaa ya namna na kuyatimiza ndani ya mwaka huo na ikiwa atapanga kufanya jambo kubwa hutamani kuona amelifanya kwa ukubwa fulani.

Wengi hujiwekea malengo ya kupiga hatua katika mambo mbalimbali kama vile kununua kiwanja, kufanikisha ujenzi, kuanzisha biashara, kuongeza viwango vya elimu na mengine mengi.

Kwa vijana wanaovuka hatua moja ya elimu kwenda nyingine nao huwa na shauku ya kufanya juhudi kimasomo ili mwisho wa elimu zao kuonja kile wanachotamani.

Katika kufanikisha maazimio hayo kila mtu hutimiza malengo anayoona yanamfaa kufanya kulingana na uwezo wake au kadiri nafsi yake inavyopenda afanye.

Kujiwekea malengo kuna faida nyingi na muhimu mojawapo ni kujiona fahari unapofanikiwa kuyatimiza.

Lakini inakupasa ufahamu kuwa ili uyatimize malengo yako, unahitajika kujiandaa mapema kwa kuweka nia madhubuti na pia mkakati wa kuyafanikisha. Kamwe usisubiri miujiza, anza sasa.

Tukutane wiki ijayo.

***Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0715 88 67 49.***



# Suruali za 'bwanga' zinavyobamba

SURUALI za bwanga zinaendelea kushika chati kila kukicha kutokana na staili yake ya kutobana mwilini na kumwacha mvaaji akiwa huru.

Ukiachana na suruali za jinzi, bwanga na shati zinafuatia kwa kupendwa na kuvaliwa kwa wingi na wanawake, hususani wale wa rika la kati.

Bwanga kwa namna ilivyo, unaweza kununua kitambaa na kushona ama kununua dukani ikiwa haibani, na ukavaa popote ikiwemo ofisini au mtoko wa kawaida.


Sifa za bwanga

*Haibani

*Inakupa nafasi ya kuwa huru

*Unaweza kuvaa na blauzi yake au kuvaa na top isiyobana.

*Unaweza kuvaa na raba au viatu virefu na ukaonekana bomba.



# Tangawizi, kitunguu vinavyokuza nywele

TANGAWIZI ni kiungo kwa vitu vingi – hasa vyakula, ikiwemo mboga na chai, lakini pia ikitumiwa vyema inaweza kusaidia kukuza nywele ambazo zimedumaa.


*Namna unavyoweza kufanya ni kuchukua tangawizi na kuchanganya na kitunguu maji kisha ukavisaga kwa pamoja.

*Chukua chujio, chuja mchanganyiko huo kisha tumia kuupaka kichwani kwa kukata mistari kisha unamasaji.

*Fanya hivyo angalau mara tatu kwa wiki utaona matokeo mazuri mapema.



# Uwoya: Niliwahi kum-DM Elon Musk



Na Mwandishi WETU

MWIGIZAJI wa Bongo Movie, Irene Uwoya amesema aliwahi kumtumia ujumbe kupitia Instagram, mfanyabiashara mkubwa kutoka Marekani, Elon Musk.

Uwoya alitoa siri hiyo hivi karibuni baada ya kuulizwa kwenye kipindi cha 'reality show,' kuwa mtu akishika simu yake ni sehemu gani ambayo hatatamani mtu afungue.

"Mtu akishika simu yangu sitaruhusu aingie kwenye DM yangu kwa sababu niliwahi kum-DM hadi mfanyabiashara mkubwa kutoka Marekani, Elon Musk,"alisema Uwoya.



# Miriam Chirwa achumbiwa

Na Mwandishi WETU

MUIMBAJI maarufu wa nyimbo za Injili nchini, Miriam Chirwa, amechumbiwa huku akionyesha furaha na shukrani kubwa kwa Mungu kwa hatua hiyo.


"Namshukuru Mungu kwa safari ya maisha na yote niliyoyapitia. Ni neema ya kipekee kwa Mungu kuniongoza hadi kumpata mtu anayenipenda na kuniheshimu,"amesema Miriam.



# Jinsi ya kusoma Pambazuko

rifaly

## Soma Gazeti la Pambazuko Popote Ulipo!




Scan QR Code
Kusoma

**Jinsi ya Kusoma Pambazuko Ndani ya Rifaly**

- **Scan QR Code** – Itakupeleka moja kwa moja kwenye channel ya Pambazuko ndani ya **Rifaly.**
- **Jisajili au Ingia (Log In)** – Tumia namba ya simu, barua pepe, au akaunti ya Google.

Furahia Kusoma Pambazuko muda wowote na mahali popote ulipo.

Pakua Rifaly Sasa
na Anza Kusoma





# Simba yafika mwisho?

Na Mwandishi WETU

SAFARI ya Timu ya Simba ya Tanzania, 'Mnyama', inaendelea kuingia kiza, hivyo ndivyo unavyoweza kusema baada ya kuchezea tena kichapo dhidi ya Espérance De Tunis ya nchini Tunisia juzi.

Simba SC wameendelea kugawa utamu kwenye Michuano ya Klabu Bingwa Afrika (CAFCL) baada ya kufungwa bao 1 dhidi ya wenyeji hao na kuifanya kuendelea kushika mkia kwenye msimamo wa Kundi D ikiwa haina alama hata moja.

Sasa Mnyama ana kibarua kizito Januari 30, 2026 kwenye mechi yake ya marudiano dhidi ya Waarabu hao ndani ya Dimba la Benjamini Mkapa, Dar es Salaam.

Swali ambalo mashabiki wengi wa Simba wanajiuliza ni hili; je, klabu yao yenye makazi yake Msimbazi, Dar es Salaam, itaweza kupindua meza na kuchukua alama tatu muhimu au ndio vipigo vitaendelea kuwaandama?

Simba amebakisha jumla ya michezo mitatu; miwili ikiwa nyumbani na mmoja ugenini dhidi ya Petro de Luanda ya Angola. Ikiwa Simba itashinda michezo yote iliyobaki, itakuwa imekusanya alama tisa.

Mbali na Simba, pia watani wao wa jadi, Yanga ya Dar es Salaam, nao walilamba kichapo kwa kufungwa mabao 2-0 dhidi ya wenyeji, Al Ahly ya Misri - nao watacheza Januari 30, 2026 kwenye Dimba la Amaan Karume, Zanzibar.

Yanga ambaye ana alama nne mpaka sasa, yupo nafasi ya pili katika msimamo wa kundi B. Bado ana matumaini ya kusonga mbele ikiwa atamfunga mpinzani wake kwenye mchezo wa marudiano.

*GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.*

TAMPA
TANZANIA MEDIA PRACTITIONERS ASSOCIATION